tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



## KESI DADA BILIONEA MSUYA
Mwanafunzi atoa ushahidi alivyopewa funguo na asiyemjua

UKURASA 4




### Mjadala mzito wa Bandari Dar na mada za uzalendo zinavyoshindana



UKURASA 11

# Nipashe
Jumatano Agosti 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581411
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Upinzani walia demokrasia, Kinana awajibu 'mnapitiliza'

UKURASA 2





UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mgeni wake Rais wa Jamhuri ya Indonesia, Joko Widodo, baada ya kuwasili Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Tanzania, Indonesia zatia saini ushirikiano mambo 7

UKURASA WA 3

### HITILAFU MFUMO UZALISHAJI UMEME TANESCO YASABABISHA 'GIZA'

HITILAFU ya mfumo katika kituo cha uzalishaji umeme kwa njia ya gesi cha Ubungo II mkoani Dar es Salaam jana imeathiri huduma nyinginezo nchini, ikiwamo maji...

UKURASA WA 5

### MATUMBO JOTO WADAIWA SUGU MFUKO WA PEMBEJEO ZA KILIMO

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeagiza Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) na Mkaguzi wa Vyama Vya Ushirika (COASCO) kupeleka orodha ya waliokopa na kutorejesha fedha, hivyo kusababisha kuwapo madeni...



KUADIMIKA DOLA

## BoT yawatoa hofu wananchi, yaja na suluhisho

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA, YANGA VITA VIKALI SAINI YA MSUVA UK. 24
KATUNI UK. 6




Vyombo vya moto vikipita kwa shida kutokana na barabara kuharibika katika makutano ya Mtaa wa Swahili na Faru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Upinzani walia demokrasia, Kinana awajibu 'mnapitiliza'

**Halfani Chusi**

WAKATI vyama vya upinzani vikisema demokrasia na uhuru wa kujieleza umeshuka, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahaman Kinana, amepinga vikali huku akisema watu wanavuka mipaka na kuvunja sheria.

Kauli hizo zilitolewa jana katika mkutano wa kitaifa uliolenga kujadili hali ya demokrasia nchini kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2025. Mkutano huo uliandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) na kukutanisha vyama vya siasa na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, alisema kama wanataka demokrasia na uhuru wa kujieleza, tiba yake ni kuwa na Katiba Mpya.

Alisema Januari, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua kamati ya kuendeleza mchakato wa Katiba Mpya na kudai mpaka sasa hakuna kinachoendelea.

"Kwa sasa kuna kitu cha ajabu. Kuna uhuru wa kujieleza lakini hakuna uhuru baada ya kutoa maelezo. Mfano mzuri ni wale ndugu zetu wanaopinga mkataba wa bandari, walikamatwa na kupewa kesi ya uhaini," alisema Mnyika.

Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo, Juma Duni Haji, alisisitiza kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi kabla ya mwaka huu kwisha ili uchaguzi ujao uwe huru, wa haki na kuaminika.

Alisema ni muhimu jambo hilo likafanyiwa kazi mapema ili uchaguzi usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi badala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mwenyekiti wa Chama cha Umma (CHAUMA), Hashim Rungwe, alisema demokrasia ya nchi imeshuka huku akisema vyombo vya dola vimekuwa na tabia ya kuingilia mazungumzo ya watu hasa yanayohusu siasa na wakati mwingine kuharibu mikutano.

Alisema wanasiasa wanaishi bila uhuru iwe nyumbani au kwenye matembezi yao ya kila siku kwa kile alichodai Jeshi la Polisi linadhani lenyewe ni CCM.

Makamu Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini, alifafanua kuwa demokrasia imeshuka kwa sababu uchaguzi unasimamiwa na upande mmoja, hakuna Tume Huru ya Uchaguzi, utaratibu unaotumika kumpata mgombea ni kama wa mchezaji na refarii.

"Uchaguzi wa serikali za mitaa unasimamiwa na TAMISEMI. Hii ni shida kwa sababu huko wamejaa viongozi wengi wa CCM unadhani watakubali kiongozi wa upinzani apite?

"Tunataka uchaguzi huo usimamiwe na tume huru, tunateswa tunapigwa na polisi wanatunyanyasa vyama vya upinzani, ndiyo maana kila siku demokrasia inazidi kudidimia," alisema.

"Ukifika wakati wa uchaguzi chama tawala kinapewa mabilioni ya fedha, lakini hivi vingine havipewi hata shilingi moja vinashindwa kufanya hata mikutano ya kisiasa hili haliko sawa," aliongeza.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Maftaha Nachuma, alisema hali ya demokrasia na uhuru wa kujieleza kwa sasa ni mbaya huku akidai umeshuka kwa kiwango kikubwa.

Alisema vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo kazi yao ni kulinda usalama wa raia na mali zao, vimekuwa vikiharibu uchaguzi ambao upo kwa mujibu wa sheria. Pia alisema vyombo hivyo vimekuwa vikitumika kupanga matokeo ya uchaguzi, watu kupiga kura zaidi ya mara mbili kwa kuwasindikiza.

Mwenyekiti wa (TCD), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema tangu mfumo wa vyama vingi ulipokubalika nchini mpaka leo, hawajafanikiwa kujenga demokrasia ya kweli huku akibainisha kuwa kuna matukio mengi yanayotokea yanadhihirisha kutokuwapo kwa hali hiyo.

"Katika uchaguzi wa mwaka 1995, wabunge wa vyama vya upinzani walipata asilimia 45 katika idadi ya wabunge 232, CCM walikuwa 186 upinzani walikuwa 46, lakini katika uchaguzi wa 2015, vyama vya upinzani vilipata wabunge 68 kati ya wabunge 257.

"Lakini uchaguzi wa mwaka 2020, vyama vya upinzani vilipata wabunge wanane tu kati ya wabunge 264. Toka tumeanza uchaguzi mkoa wa Kilimanjaro, ulikuwa unatoa wabunge toka vyama vya upinzani lakini mwaka huo hakukuwa na mbunge hata mmoja.

"Ni wazi kabisa hii ilikuwa sunami ya uchaguzi na hili jina la sunami alilitoa mtani wangu, Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, ndiyo alisema kwa mara ya kwanza kwamba, matokeo hayo ni sunami ya uchaguzi," alisema Lipumba ambaye ni Mwenyekiti wa CUF.

Alisema kuwa hali hiyo si njema, inaonyesha dhahiri hakuna demokrasia ingawa anakiri alipoingia Rais Samia, angalau kidogo kauli zake ziliwapa matumaini kwa kauli yake kuwa "nchi hii ni yetu sote".

Prof. Lipumba alisema CUF kimekuwa kikitoa ushauri kwa Rais Samia akimaliza kipindi chake, aweze kupata tuzo ya Mo-Ibrahim.

Alisema Rais anatakiwa kuendesha nchi kidemokrasia, kulinda haki za binadamu, kupambana na rushwa pamoja na kukuza uchumi shirikishi wa kupambana na umaskini.

**KINANA AJIBU**

Akijibu hoja za wapinzani, Kinana alisema demokrasia na uhuru wa kujieleza bado upo juu huku akikubali kuwapo kwa upungufu katika kusimamia sheria kuwa kuna sehemu serikali inateleza.

Alisema uhuru wa kujieleza upo ingawa watu wamekuwa wanavuka mipaka na kuvunja sheria za nchi huku akikiri kuwa kuna kasoro katika utekelezaji wake watu wanapopitiliza hasa namna ya kuwadhibiti.

"Tangu Rais Samia aingia madarakani juhudi mbalimbali zimeanza kufanyika, mtakumbuka alipopokea tu kijiti alianza kuongelea mchakato wa katiba mpya. Aliweka mkakati wa kugusa maeneo matatu ikiwamo tume huru ya uchaguzi, uchaguzi wenyewe pamoja na namna vyama vya siasa vitakavyosimamia uchaguzi," alifafanua Kinana.

## Tanzania na Indonesia zatia saini kushirikiana mambo 7

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA na Indonesia zimetia saini hati za ushirikiano katika maeneo saba ambayo ni afya, nishati, madini, uchumi wa buluu, biashara na uhamiaji.

Nchi hizo pia zimekubaliana kushirikiana katika masuala ya siasa na kiuchumi pamoja na kukuza uwekezaji.

Katika mkutano na waandishi wa habari Ikulu, jijini Dar es Salaam jana baada ya utiaji saini wa makubaliano hayo uliofanywa na mawaziri na viongozi waandamizi wa nchi hizo, Rais Samia Suluhu Hassan alisema uhusiano wa Tanzania na Indonesia ulianza mwaka 1965.

"Uhusiano wa Tanzania na Indonesia ulianza zamani sana, tangu utawala wa Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Rais wa kwanza wa nchi hiyo, Sukarno. Kwa miaka yote nchi hizi zimekuwa zinashirikiana kwa ukaribu. Ubalozi wa kwanza kufunguliwa hapa nchini baada ya Muungano ulikuwa wa Indonesia," alisema.

Rais Samia alisema kuwa wakati wa mazungumzo na mgeni wake (Rais wa Indonesia), Joko Widodo, walikubaliana kushirikiana katika sekta mbalimbali, mojawapo ni kukuza uchumi wa digitali.

Alisema pia wamekubaliana kuendeleza na kuziweka pamoja sekta binafsi za nchi hizo.

Rais Samia alisema pia wamekubaliana kushirikiana katika kuendeleza viwanda, kilimo, uvuvi, uchimbaji wa mafuta na gesi, nishati, madini na utalii.

"Kwenye mazungumzo yetu pia nimemwomba ushirikiano katika kukuza uwezo na ujuzi katika kilimo, ushirikishwaji wa sekta binafsi, ufanisi wa mashirika ya kibiashara, uchumi wa digitali pamoja na kuongeza uwezo wa rasilimali," alisema Rais Samia.

Naye Rais wa Indonesia, Widodo, alisema nchi yake kwa sasa inajipanga kufanya uwekezaji Afrika, hususani Tanzania.

Alisema wamefurahi kushirikiana na Tanzania katika sekta mbalimbali hususani katika uchimbaji wa gesi asilia eneo la Madimba, mkoani Mtwara.

Rais Widodo alisema Indonesia itaendelea kuiunga mkono Tanzania hususani katika masuala ya maendeleo.

Pia, alisema watahakikisha mikataba iliyotiwa saini, inakuwa na taji na kuahidi kuunga mkono juhudi za serikali katika sekta ya gesi asilia na kufufua mradi wa kilimo mkoani Morogoro.

Rais Widodo alisema: "Indonesia inamhakikishia Rais Samia kuwa tutazisaidia nchi zinazoendelea kwa kufanya uwekezaji katika miradi ya maendeleo kwa maslahi ya kiuchumi."

Rais Samia aliridhia uamuzi wa Serikali ya Indonesia wa kufufua shughuli za Kituo cha Mafunzo ya Kilimo kwa Wakulima Vijijini (FARTC) kilichoko Mkindo, mkoani Morogoro.

Alisema kituo hicho kilichoanzishwa mwaka 1996 na Serikali ya Indonesia, kimechangia kwa kiasi kikubwa kuelimisha wakulima na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa kilimo.

HABARI KITAIFA



Mamalishe wakifanya biashara katika mazingira machafu kando ya barabara ya Soldering, Mikocheni Viwandani, Dar es Salaam jana kitendo kinachohatarisha afya za walaji. **PICHA: GIFTY KENNY/UDSM**

# BoT yawatoa hofu wananchi upungufu dola, yaja na suluhisho

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema ina akiba ya kutosha ya fedha za kigeni zinazoweza kutosheleza kwa miezi mitano na kutaja mikakati ya kukabiliana na upungufu wa fedha hizo nchini.

Akiongea na wahariri na waandishi wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Utafiti na Sera wa BoT, Suleiman Misango, alisema hadi kufikia Agosti 21, mwaka huu ilikuwa na akiba ya Dola milioni 5.441 (Sh. bilioni 5.441) kiasi ambacho kinalingana na kipindi kabla ya changamoto za uchumi wa dunia zilizosababisha kuwapo kwa upungufu wa fedha za kigeni nchini.

Kiwango cha fedha za kigeni kilichopo nchini kwa upande wa dola ya Marekani ni asilimia 77, Yuan ya China (16%), Pound ya Uingereza (4.78%) na dola ya Australia (1.72%).

Misango alikuwa akizungumzia mwenendo wa hali ya fedha za kigeni nchini na hali iliyochangia upungufu wa Dola za Kimarekani, mkutano ambao pia ulihudhuriwa na wafanyakazi wa benki mbalimbali za biashara na wamiliki wa maduka ya kubadili fedha za kigeni nchini.

"Miezi mitano tunaweza ku-survive (kutumia) na BoT inatarajia kuongeza ukwasi ili kupunguza changamoto zilizopo na hali inaendelea kutengemaa," alihakikisha.

Akitaja mikakati iliyochukuliwa kukabiliana na tatizo hilo, alisema BoT inatarajia kuendelea kutumia akiba hiyo kuongeza ukwasi katika soko la fedha za kigeni nchini. Kuanzia mwezi Julai hadi Agosti 21, mwaka huu BoT imeuza katika soko la fedha za kigeni dola milioni 100.5 ikilinganishwa na dola milioni 62 katika kipindi cha Julai – Septemba, mwaka jana.

Mkakati mwingine ni BoT kuongeza kiwango cha kuuza fedha za kigeni katika soko la fedha hizo, kuongeza vyanzo vya upatikanaji wa fedha hizo ikiwamo ununuzi wa dhahabu na mikakati ya kuongeza mauzo nchi za nje na kuzalisha bidhaa mbadala wa zile zinazoagizwa nje ya nchi.

Benki Kuu pia inaendelea kushirikisha benki, maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, pamoja na wadau wengine katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya fedha za kigeni nchini.

"Hatua hizo zimeanza kuleta mafanikio, ikiwamo kupunguza kasi ya mabadiliko katika thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani katika soko la rejareja," alisema.

Katika tathmini iliyofanywa na BoT, uchumi wa dunia umeanza kuimarika na kuashiria kuanza kuwapo kwa ongezeko la fedha za kigeni nchini, hususan kuanzia mwishoni mwa mwaka 2022.

"Ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kufikia asilimia tatu mwaka 2023 tofauti na matarajio ya awali ya ukuaji wa asilimia 2.8. Bei za bidhaa katika soko la dunia zimeendelea kupungua," alisema.

Aidha, alisema uchumi wa Tanzania unaendelea kuimarika na kuna viashiria vya kupungua kwa changamoto za upungufu wa fedha za kigeni nchini na mwelekeo ni kuongezeka kwa fedha za kigeni nchini.

BoT inatarajia upatikanaji wa fedha za kigeni hususan dola ya Marekani kuimarika katika siku zijazo kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali na Benki Kuu za kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni nchini.

Hata hivyo, BoT imesisitiza katazo lake la wananchi kupanga bei na kufanya malipo kwa kutumia fedha za kigeni hususan dola. Benki hiyo imewataka wafanyabiashara fedha zitokanazo na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kuwekwa katika benki za nchini ndani ya siku 90 tangu siku ya kusafirishwa kwa mujibu wa Kanuni ya Fedha za Kigeni, 2022, kanuni 7(4) lengo likiwa ni kuongeza ukwasi wa fedha za kigeni nchini.

Pia wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kutoka nje kufanya malipo kwa kutumia benki na taasisi za fedha nchini, shughuli za kununua au kuuza fedha za kigeni nchini zinatakiwa kufanyika na taasisi za fedha zilizoidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania pekee.

BoT imewataka wananchi kuongeza matumizi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini ili kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni, kuimarisha shughuli za uchumi na kuongeza kipato kwa wananchi.

Mhazini kutoka Benki ya NMB, Aziz Chacha, alipendekeza wafanyabiashara kutumia sarafu mbadala wanapoagiza bidhaa nje ya nchi na kutoa mfano kama bidhaa inanunuliwa Afrika Kusini inunuliwe kwa fedha ya nchi hiyo ambayo ni Rand na kama India inunuliwe kwa Rupia, ili kupunguza matumizi ya dola ya Marekani.

# Hitilafu mfumo uzalishaji umeme TANESCO yasababisha 'giza'

**Na Elizabeth Zaya**

HITILAFU ya mfumo katika kituo cha uzalishaji umeme kwa njia ya gesi cha Ubungo II mkoani Dar es Salaam jana, imeathiri huduma nyinginezo nchini, ikiwamo maji.

Wakati Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) likieleza jitihada zake kukabiliana na tatizo hilo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imesema kasoro hiyo imekwamisha huduma zake kuzalisha maji katika mitambo yake mikuu ya Ruvu Juu, Ruvu Chini, Wami na Mtoni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma TANESCO, hitilafu hiyo ilisababisha upungufu wa uzalishaji umeme kwa jumla ya megawati 268 kutokuwa katika mfumo wake wa usafirishaji.

"Hivyo, baadhi ya maeneo kwenye mikoa nchini yanakosa huduma ya umeme kwa nyakati tofauti. Jitihada za kurekebisha tatizo hilo zinaendelea na tutawataarifu wateja wetu kila baada ya saa nne kadri hali ya upatikanaji wa huduma itakavyokuwa inaimarika.

"Shirika linawashukuru wateja wake kwa uvumilifu katika kipindi chote ambacho huduma ya umeme inakosekana," TANESCO ilibainisha katika taarifa yake hiyo.

Ilipotimu alasiri, shirika hilo kupitia kwa Kaimu Mkurugenzi Huduma kwa Wateja, Martin Mwambene, lilitoa taarifa likiahidi huduma kurejeshwa kabla ya siku kuisha.

"Kama tulivyotangaza katika matangazo yetu usiku wa kuamkia leo (jana), kituo cha Ubungo II kinachozalisha umeme kwa njia ya gesi, kilipata hitilafu katika mifumo yake na hivyo kusababisha megawati 268 kukosekana. "Jambo la kuwaambia wananchi ni kwamba, mafundi wetu tayari wapo katika eneo hili wakifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha mfumo huu unarejea katika hali yake ya kawaida.

"Tunajitahidi kurejesha huduma ya umeme kabla ya siku ya leo (jana) kuisha. Tunaendelea kuwashukuru kwa uvumilivu wenu wakati tukiendelea na jitihada hizi za kurejesha huduma kama ilivyokuwa mwanzo," alisema.

**DAWASA**

Taarifa ya DAWASA iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Jamii jana, ilibainisha kuwa kasoro hiyo imeathiri shughuli za uzalishaji maji katika mitambo yake ya uzalishaji maji Ruvu Juu, Ruvu Chini, Wami na Mtoni.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa changamoto hiyo imesababisha upungufu wa upatikanaji huduma ya maji katika maeneo mbalimbali ya huduma Dar es Salaam na Pwani.

"Sababu ni hitilafu ya mfumo wa umeme katika kituo cha uzalishaji umeme kwa njia ya gesi cha Ubungo II, kinachosimamiwa na TANESCO.

"Mamlaka inawakumbusha wananchi kuhifadhi maji katika kipindi hiki. Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza, upatikanaji wa huduma utarejea katika hali yake ya kawaida mara tu tatizo la umeme litakapotatuliwa," DAWASA ilieleza katika taarifa hiyo.


AFFAIRES INTERNATIONALES
TOUR DEFENSE PLAZA
23-27 rue Delarivière Lefoullon,
CS 90132, 92064 LA DEFENSE CEDEX
France

Date: 10th of August 2023

**OTIS DISTRIBUTOR IN TANZANIA**

To whom it may concern

**CERTIFIED LETTER**

Whereas **OTIS GDN** (Global Distributor Network) who are official manufacturers of LIFTS, having our Headquarter at 23-27 Rue Delarivere Lefoullon, 92064 LA DEFENSE do hereby confirm that:

**DERM ELEVATORS LIMITED**
**Sky City Mall, 11th Floor,**
**University Road**
**Plot 403/1-2 Block A, Mlalakuwa**
**Dar es salaam, Tanzania**

Website: www.derm.co.tz email: elevators@derm.co.tz
Tel: +255 22 2774507

Is an OTIS authorized distributor for TANZANIA territory.

DERM ELEVATORS LIMITED is authorized to promote, sell, install, and adjust elevators, escalators and travolators manufactured by OTIS Elevator Company.

Acting as distributor, DERM ELEVATORS LIMITED is benefitting from the commercial, technical and logistic support from OTIS Elevator Company and DERM ELEVATORS LIMITED technicians have received a specific training by OTIS to perform the installation and the maintenance of OTIS' product range.

*POLTORAK Thomas*
*Area Manager*

OTIS Affaires Internationales TOUR DEFENSE PLAZA 23-27 rue Delarivière Lefoullon CS 90132 92064 LA DEFENSE CEDEX

Derm Elevators

Siège Social Otis
SCS au Capital de 6.202.305€
otis.com

Tour Défense Plaza
23-27 rue Delarivière Lefoullon
92800 Puteaux
Tel : 01 46 91 60 00

SIREN 542.107.800 RCS Nanterre
APE 4329B
N° TVA : FR 72 542 107 800

OTIS

# Mwanafunzi atoa ushahidi kortini alivyopewa ufunguo na asiyemjua

**Na Grace Gurisha**

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Al- Rahmah, Aziza Mohamed (16), ameieleza mahakama katika kesi ya mauaji ya mdogo wa marehemu, Erasto Msuya maarufu kama Bilionea Msuya, Aneth Msuya, alivyopewa funguo na mwanadada asiyemfahamu na kumwelekeza kuupeleka nyumbani kwa kina Iliamu.

Mwanafunzi huyo ambaye ni shahidi wa 19 katika kesi hiyo, alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake akiongozwa na Wakili wa Serikali, Generosa Montana.

Washitakiwa katika kesi hiyo namba 103 ya mwaka 2018 ni mke wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu wa madini mkoani Arusha, marehemu Erasto Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela wote wakazi wa mkoani Arusha.

Alidai kuwa anaishi Kibada Kigamboni na baba, mama, wadogo zake wawili na kaka yake na sasa ana miaka 16 na yuko kidato cha tatu katika shule hiyo.

"Mwaka 2016 nilikuwa nasoma Shule ya Msingi Bethania darasa la tatu nikiwa na miaka tisa. Nilikuwa naishi Kibada Kigamboni block 16," alidai Mohamed.

Alidai kuwa Mei 25, 2016 anakumbuka majira ya saa 10:00 jioni alikuwa anatoka shuleni Kwenda nyumbani, njiani alikutana na dada mfupi maji ya kunde akiwa amebeba kipochi na alimwambia achukue ufunguo aupeleke nyumbani kwa kina Iliamu.

"Baada ya kunikabidhi ufunguo nilikwenda kwa kina Iliamu. Nilipofika nikamkabidhi Aliamu Marino ambaye ni tumbo moja, nikamwambia ufunguo nimepewa na mdada simjui, basi nikaondoka kurudi nyumbani," alidai Mohamed.

Alidai kuwa Iliamu na Aliamu wanaishi Kibada Kigamboni, Bloki 17 na pia wakati alipokabidhiwa ufunguo huyo dada alikwenda mtaani kwao na yeye alikwenda kwa kina Iliamu.

Akijibu maswali ya upande wa utetezi kutoka kwa mawakili Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko, Mohamed alidai kuwa kabla ya kuampa hakuelezwa kama anaelewa maana ya kiapo.

Pia alidai kuwa huyo dada ambaye alikutana naye hamjui na pia hafahamu marehemu Aneth Msuya na wakati akitoa ushahidi wake hakuambiwa afafanue kuhusu ufunguo yeye aliambiwa aupeleke tu.

Shahidi namba 20, ambaye ni mjasiliamali wa kuuza chipsi, Nasibu Idriano, alidai kuwa Agosti 21, 2016 aliombwa na Askari polisi ashiriki katika gwaride la utambuzi wakati akiwa Kituo cha Polisi Kilwa Road kumfutilia mtoto wa dada yake aliyekamatwa.

Alidai kuwa alikubaliana na ombi hilo na alipelekwa nyuma ya kituo hicho, alikutana na wenzake ambao wanafanana kwa rangi na urefu sawa, msimamizi wa gwaride aliwaomba waridhie kwa Pamoja na walilidhia.

"Wakati tumepanga mstari mmoja alikuja askari mmoja akiwa na mtuhumiwa wa kiume. Alimwambia kuwa na amani na kuwa huru kuchague sehemu yoyote unayotaka kukaa," alidai Idriano

Pia, aliambiwa anaweza kubadilishana na mtu shati, baada ya askari kumaliza kusema hayo mtuhumiwa aliomba wabadilishane fulana na yeye akakubaliwa, alikaa upande wake wa kulia na kutoka kushoto ni wa pili. Kulia kwake mtuhumiwa alikuwa namba nane na yeye alikuwa wa tisa.

Alidai kuwa aliletwa dada mfupi maji ya kunde na kuelezwa kuwa anatakiwa apite kwenye mstari mbele na nyuma na akishamtambua mtuhumiwa amshike bega na dada huyo alifanya hivyo kwa kumshika bega.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Marietta Maguta, shahidi alitakiwa atazame watu wote waliyokuwa kwenye ukumbi wa wazi wa mahakama ili aionyeshe mahakama kama mtuhumiwa aliyetambuliwa kwenye gwaride yupo.

**Shahidi**: Naomba avue barakoa ili niweze kumtambua.

**Jaji:** Ni yupi huyo.

**Shahidi:** Ni huyo hapo mbele.

**Jaji:** Kama kuna mtu yeyote humu ndani amevaa barakoa avue.

Baada ya kauli hiyo ya Jaji, mshitakiwa wa pili, Muyela ndiye aliyekuwa amevaa barakoa peke yake. Aliangalia pande zote za chumba cha mahakama ndipo akaivua.

**Shahidi:** Ni yeye sema kwa sasa amepungua sana.

**Muyela:** Nivue na miwani.

**Shahidi:** Hapana.

Akijibu maswali ya mawakili Kibatala na Nkoko, shahidi huyo alidai kuwa hakumwambia jaji rangi ya nguo ambayo alikuwa amevaa na pia hakueleza mahakama kama kipindi hicho mtuhumiwa alikuwa anavaa miwani.

**Kibatala:** Una futi ngapi?

**Shahidi:** Nina futi tano.

**Kibatala:** Na point ngapi.

**Shahidi:** Sijapima muda mrefu.

**Kibatala:** Unafahamu kama mtuhumiwa ni futi sita?

**Shahidi:** Ndiyo alinipita urefu.

**Nkoko:** Ni kweli ulisema mnalingana urefu na rangi katika ushahidi wako?

**Shahidi:** Ni kweli ila sasa nimenenepa nimeshuka kidogo.

**Nkoko:** Ni kweli hukuiambia mahakama kwamba wote mlikuwa saizi moja ya mwili?

**Shahidi:** Ni kweli

**Nkoko:** Katika ushahidi wako ulisema gwaride lilianza saa tano asubuhi lakini kwenye hii karatasi imejazwa saa 6:49 mchana. Kwa hiyo ulikuwa unaidanganya mahakama?

**Shahidi:** Kwa mujibu wangu hilo ni suala la askari aliyeandika.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi leo saa 3:00 asubuhi. Shahidi wa 21 wa upande wa mashtaka atatoa ushahidi wake. Hata hivyo, Jaji Kakolaki aliutaka upande wa mashtaka kupeleka mashahidi wengi ili kuokoa muda.


The Guardian Limited

JOB VACANCY

The Guardian Limited, **Publishers of leading Tanzanian newspapers, The Guardian, Nipashe and Nipashe Jumapili, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**SENIOR MARKETING EXECUTIVE - DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**

Developing and executing strategies to promote brands, products and services, maximizing profits for the company.

**Main Responsibilities:**

- Formulate an appropriate commercial strategy that responds to the overall development of the company's marketing operations, newspaper sales, advertisements and other printed products.
- Become knowledgeable expert of The Guardian Limited products and be experienced in identifying target markets and developing strategies to communicate with them.
- Identify, plan, prepare and produce proposals for the targeted audiences.
- Study competitors' products and services on a daily basis, with a view to designing counter strategies.
- Advise clients on their advertising and promotion campaigns.
- Organize all company events related to CSR, promotion, product launching, staff parties, etc.
- Monitor and analyze product performances, trends and provide accurate reports on programe and market information.
- Explore ways of improving existing products and services and increasing profitability.
- Advise the Management with feasibility studies on ways to get sponsorship for various events, highlighting benefits to the Company.
- Engage in negotiating and closing deals where and if appropriate.
- Prepare periodic performance reports for the Management and provide appropriate inputs towards improvement and the taking of remedial measures.
- Design and implement human resources training and development programme

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 5 years' relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge and familiarity with a wide range of newspaper brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via email address: vacancy@guardian.co.tz by **8th September, 2023.**

**NB:** Only shortlisted candidates will be contacted.

***Please note that The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

# Matumbo joto wadaiwa sugu Mfuko wa Pembejeo za Kilimo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeagiza Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) na Mkaguzi wa Vyama Vya Ushirika (COASCO) kupeleka orodha ya waliokopa na hawajarejesha fedha, hivyo kusababisha kuwapo madeni chechefu ya Sh. bilioni 20.

Baada ya jana kuhoji utekelezaji wa hoja za ukaguzi za mwaka 2021/22 kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Mfuko na Mkaguzi huyo (COASCO), Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, aliwaambia waandishi wa habari kuwa kamati imesikitishwa kuwapo madeni chechefu makubwa.

Alisema, madeni hayo yanayotishia uhai wa mfuko na kuagiza orodha hiyo iwasilishwe leo kabla ya saa saba mchana katika Ofisi ya Katibu wa Bunge.

"Mfano, kati ya Sh. bilioni 26 ambazo mfuko ulikuwa utumie katika kutoa mikopo, Sh. bilioni 20 ni madeni chechefu ambayo hayawezi kukusanyika. Hii ni sawa na asilimia 83 ya fedha zilizotolewa ambazo hazijawahi kukusanywa,"alifafanua.

Aliongeza: "Ukiangalia mfuko huu wa pembejeo ambao hautoi pembejeo, unatoa mkopo. Hizi ni fedha za walipakodi ambazo wameshindwa kuzikusanya. Kuna ufanisi wa huu mfuko kweli? Ukiangalia kazi za Benki ya Kilimo na mfuko wanafanya kazi inayofanana, kuna sababu gani kuwa na benki na mfuko huu?"

Kuhusu Benki ya TADB, alisema wajumbe PAC wameonesha wasiwasi mkubwa baada ya kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kuhoji benki hiyo inavyowafikia wakulima wadogo.

"Wasiwasi wa wanakamati ni kwamba, wakulima wale wadogo ambao ndio lengo la kuanzishwa benki hii hawafikiwi na badala yake wanapewa wale wakubwa ambao wangeweza kutumia benki za kawaida za biashara. Kwahiyo, kuna tatizo kubwa la kukiuka madhumuni ya kuanzishwa kwa benki hii.

"Benki hii imekuwa inapitisha fedha zake nyingine katika benki nyingine za biashara ili zile benki ndio ziwape wakulima. Sasa unajiuliza hiyo gharama nani anaibeba, maana benki inayopewa itoe fedha kwa wakulima itaweka riba. Hii benki yenyewe ya kilimo inaweka riba yao, haya yote yanakwenda kwa mkulima,"alisema.

Kaboyoka pia alihoji sababu za benki hiyo kutumia fedha za umma kupeleka benki nyingine ili wakulima wakachukue huko na kupambana na riba zingine.

Mwenyekiti huyo pia alisema kamati imeona COASCO wanapofanya ukaguzi na kukabidhi ripoti kwa vyama vya ushirika, hakuna wa kuchukua hatua.

"Inawezekana COASCO utendaji kazi wake usionekane umuhimu wake kama wanatoa ripoti inatolewa na haifanyiwi kazi na mtu yeyote, ule upungufu haufanyiwi kazi," alisema.

Kaboyoka alisema kuna umuhimu ripoti za COASCO zifanyiwe kazi kama ilivyo katika kufanyia kazi hoja za CAG zinapopelekwa bungeni ili kuwa na tija.

## Pacha wa Tabora walioungana sasa kutenganishwa Saudi Arabia

**Na Anjella Mndolwa,** TUDARCo

SERIKALI ya Saudi Arabia imesema itasaidia na kusimamia matibabu ya kutenganisha watoto waliozaliwa wakiwa wameungana, Hussen na Hassan wenye umri wa mwaka mmoja na miezi 11, wakazi wa Mkoa wa Tabora wanaoendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alibainisha hayo jana alipozungumza na Kaimu Balozi wa Saudi Arabia nchini, Fahad Alharbi, aliyefika hospitalini huko kwa lengo la kuwajulia hali na kuwaaga watoto hao.

Watoto hao wanatarajiwa kuondoka Tanzania leo nchini kuelekea Saudi Arabia kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji wa kutenganisha.

Prof. Janabi alisema MNH ina uwezo wa kufanya upasuaji wa aina hiyo kwa kuwa ina miundombinu na wataalamu iliyojitosheleza, lakini kutokana namna watoto hao walivyoungana, inahitaji utaalamu zaidi.

"Tumekuwa na watoto hawa kwa miezi 11, wameungana kwenye nyonga, kifua na wana miguu mitatu, upasuaji kuwatenganisha ni mkubwa zaidi hivyo, kesho (leo) timu ya wataalamu wa MNH ikijumuisha madaktari wa upasuaji na wauguzi itaondoka na watoto hawa kuelekea Saudi Arabia kwa ajili ya upasuaji," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto wa MNH, Dk. Zaitun Bhokhary, alisema watoto hao walipokewa MNH wakiwa na umri wa wiki mbili na walikuwa na changamoto mbalimbali za kiafya ambapo wamepatiwa matibabu na kutunzwa hadi kufikia hatua ya kupelekwa katika nchi hiyo kwa ajili ya upasuaji huo.

"Kama ambavyo Profesa (Janabi) amesema, hawa watoto wameungana sehemu kubwa (complex conjoined twins), hivyo upasuaji wake utahitaji utaalamu zaidi," alisema Dk. Zaitun.

Alisema wataalamu wa MNH watakaoambatana na watoto hao huko Saudi Arabia, wataruhusiwa kushiriki katika upasuaji na matibabu, jambo ambalo litasaidia kuwajenga uwezo.


**TOL Gases Limited** We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

# NOTICE

## 28TH ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** the 28th Meeting of the Shareholders of TOL Gases Limited will be held on a hybrid of physical attendance at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) and via ZOOM video conferencing on 25thAugust, 2023 at 9.00a.m to transact the following business:-

1. Adoption of the Agenda.
2. Confirmation of Minutes of the year 2021 Annual General Meeting held on 19th August, 2022.
3. Matters arising from minutes of the year 2021 Annual General Meeting.
4. Chairman's Statement.
5. To receive Directors' Report, Auditors' Report and the Audited Financial Statements for the year ended December, 31, 2022.
6. To approve Dividend Payment.
7. To approve Directors' Fees.
8. To appoint Auditors for the year 2023.
9. Election of Directors.
1. To set the place, date and venue of the next meeting.
1. Any other business (Duly notified at least seven days before the meeting)

Registration for participating in the ZOOM Video Conferencing should be done through phone no **0685750201/0685750203.**

member entitled to attend and vote at the Meeting is also entitled to appoint a proxy (whether a member of the Company or not) to attend and vote in his/her stead.

All proxy forms or letters appointing proxy must be lodged at the office of the Company Secretary at least 48 hours before the time fixed for the holding of the meeting or via email to **mjuliana@tol-gases.co.tz/nlulu@tol-gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**
**COMPANY SECRETARY**

Directors: S. Mponji – (Tanzanian) – Chairman, J. Massawe – (Tanzanian), S. Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian), L.C. Kitoka – (Tanzanian).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Unyanyasaji huu wa wanaume sasa ni mwafaka upatiwe tiba

**KATIKA** siku za karibuni, kumekuwapo na taarifa za unyanyasaji wa kijinsia wanaofanyiwa wanaume na wenzi wao zikiwamo za kunyimwa unyumba kwa sababu hawana kipato na kupata vipigo kwa kile kinachodaiwa kutoa taarifa za kuwapo kwa biashara haramu ya pombe aina ya gongo na dawa za kulevya.

Matukio hayo yameripotiwa katika mafunzo yanayofanywa na shirika lisilo la kiserikali la KIWECO la mkoani Kilimanjaro. Katika makongamano na mikusanyiko hiyo, wanaume wamejitokeza hadharani kudai kunyimwa haki zao katika ndoa ikiwamo ya unyumba kwa kile kinachodaiwa hawana kipato.

Bila kuficha maneno, baadhi ya wanaume hao wamedai kuwa wamekuwa wakinyimwa tendo la ndoa na wake zao kwa madai kwamba wamechoka kuzalishwa watoto mfululizo na kwamba sasa wamegeukia kwenye uzalishaji mali ili kujipatia fedha kwa ajili ya familia zao. Katika moja ya mikutano hiyo, baadhi ya wanaume walidai kuwa ili kupata tendo la ndoa kutoka kwa wake zao lazima watoe fedha kwanza vinginevyo hawapati haki hiyo.

Hata hivyo, mwanamke mmoja katika moja ya mikusanyiko hiyo, akiwakilisha kilio kama hicho kwa niaba ya wenzake, alikiri wazi kwamba wamekuwa wakibeba ujauzito lakini wakati wa kwenda kujifungua wanaume hawaonekani na hawashiriki katika suala la malenzi ya watoto.

Kwa maneno mengine, wanafanya hivyo kwa kuwa wamechoka kuhangaika peke yao kuanzia ujauzito hadi matunzo ya watoto. Kutokana na hali hiyo, wameamua kuwafanyia hivyo wenzi wao kama sehemu ya kuwapa funzo kwamba suala la ndoa si kuwabebesha ujauzito na kuwaacha wake zao wakihenya kutunza watoto tangu wakiwa wadogo hadi kuwasomesha.

Mbali na hilo la kunyimwa unyumba, kuna mkasa ulioripotiwa jana kuwa katika Kijiji cha Maring'a, mwanamume aliyetambuliwa kwa jina la Godlisten Shao, amejeruhiwa kwa vipigo na mke wake sehemu mbalimbali za mwili baada ya kutoa taarifa kuhusu biashara anayoifanya ya pombe haramu ya gongo na dawa za kulevya aina ya bangi.

Kutokana na vipigo anavyopata kutoka kwa mwenzi wake huyo, mwanamume huyo amedai kuwa anaishi kwa hofu kutokana na kuchangiwa vipigo kutoka kwa wateja wa mke wake huyo kwa kile wanachodai wanamfanya hivyo ilia ache kiherehere cha kufuatilia mambo ya mke wake.


Kwa ujumla, matendo hayo yametia doa kwa wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro hususan Wilaya ya Moshi. Ni dhahiri kwamba watu hao ambao wengi wao wamefunga ndoa halali na kwa hiari, waliapa kuwa watakuwa na upendo na wako tayari kuishi kwa hali zozote, za utajiri na umaskini hadi kifo kitakapowatenganisha. Sasa inakuwaje inafika hatua ya kunyimana haki za msingi katika ndoa?

Suala hili la ukatili mpya wa kijinsia ulioibuka sasa unatoa picha isiyo nzuri katika baadhi ya familia kutokana na ukweli kwamba ndoa siku zote zinajengwa kwa upendo na ushirikiano na pindi inapotokea kutokuelewana, watu wa kwanza kufanya suluhu ni wanandoa wenyewe. Lakini sasa mambo yamebadilika na siri za ndani zinatolewa hadharani na kuifanya jamii kubaki vinywa wazi.


Ni vyema sasa ufike wakati vitendo hivi vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia vipatiwe tiba ili kunusuru maisha ya ndoa na familia kwa jumla. Ndoa inapokumbwa na misukosuko, husababisha mparaganyiko baina ya wanandoa na matokeo yake wanaoteseka ni watoto.

Wakati uumefika sasa wanadoa kurejea katika misingi ya upendo badala ya ukatili mpya ulioibuka na kuzifanya ndoa kuwa katika mmomonyoko. Ni vyema wanandoa pia wakakumbuka kwamba ndoa imara huzaa jamii imara na jamii imara huzaa taifa imara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Anneth Domisian, UDSM

# Harufu, maji machafu na taka kero kubwa mtaani Mikocheni

**IMEKITHIRI** na hatari, lakini ndio hivyo tena watu wamegeuza mitaro ya maji machafu kuwa dampo ndani ya Dar es Salaam.

Harufu mbaya inayotokana na maji machafu yanayopita katika mitaro ya maji taka katika eneo la Mikocheni, Dar es Salaam imetajwa kuwa kero ya muda mrefu inayowasumbua wananchi na wanaopita maeneo hayo.

Watu wanaopita maeneo hayo, pamoja na wakazi wamelalamika kwani bomba lililopita katikati ya mtaro umefanya mtaro uzibe na kusababisha maji kutwama kwa muda mrefu huku ukitoa harufu.

Pia, mitaro imekuwa na taka mbalimbali ambazo huzalishwa na wakazi na watu wanaopita maeneo hayo, hivyo kusababisha mitaro kuwa michafu zaidi.

Vilevile, kumekuwapo kero kwa Mama Lishe wanaopika chakula pembezoni mwa mitaro hiyo, kutokana na nzi na wadudu kutoka kwenye mitaro ya maji machafu na kwenda kutua kwenye vyakula vyao hali ambayo ni hatari kwa wateja wanaokula mahali hapo, kwani uwezekano wa kupata maradhi kama kuhara ni mkubwa mno kutokana na kula vyakula ambavyo si visafi.

Mama lishe wa eneo hilo wanaiomba mamlaka husika kuondoa bomba lililopita katikati ya mtaro huo ili maji machafu yasiwe yanatuama na kutoa harufu.

Pia, wanaomba wamiliki viwanda vilivyo pembezoni na mitaro hiyo, wawe wanashirikiana katika kufanya usafi kwenye mitaro hiyo angalau mara moja kwa wiki na sio kuwaachia Mama Lishe kufanya usafi wenyewe na kuingia gharama ya kuwalipa watu kusafisha mtaro huo.

Siah Marley, ni mwanafunzi kutoka Chuo cha Kodi (ITA) kilichoko Mikocheni, anaeleza kuwa mitaro ya maji machafu kwa sasa imefanywa dampo kwani katika mitaro kuna kila aina ya uchafu ambao ndio unasababisha mitaro kuziba na maji kutwama.

Anashauri, ni vyema watu wakawa wastaarabu na kuacha kutupa taka ambazo ndio chanzo za kuziba kwa mitaro hiyo.

Wakazi wengine wa maeneo ya Mikocheni, wanasema mitaro ambayo ina maji machafu yenye harufu mbaya huwa yanatoka katika viwanda ambavyo vipo maeneo hayo.

Ni hali ambayo imesababisha kero kwa wanaotumia barabara hiyo na wafanyabishara pembezoni, huku chanzo kikiwa ufunguliaji wa maji machafu kutoka viwandani.

Jambo jingine, wananchi nao wanatakiwa wawe na uelewa juu ya umuhimu wa mitaro iliyoko pembezoni mwa barabara, kwani imejengwa kwa ajili ya kupitisha maji kipindi cha mvua, bila ya mitaro hiyo maji yangekuwa yanajaa barabarani.

Hivyo, ni muhimu mitaro ikatunzwa vizuri na sio kufanywa sehemu ya kutupa taka au kuichafua kwa namna yoyote ile.

Taka ngumu zinazozalishwa zitafutiwe sehemu maalumu pa kuwekwa kwa ajili ya kwenda kutupwa na mamlaka husika na sio kutupwa hovyo kwenye mitaro.

Mama Lishe wanaouza vyakula pembezoni mwa mitaro hiyo, ni budi nao wahakikishe sehemu wanazouzia vyakula ni safi na salama kwa ajili ya wateja wao.

Vilevile kuna haja wakawa na vyombo maalumu vya kuwekea uchafu unaozalishwa katika eneo hilo ili uchafu usitupwe mitaroni.

Mamlaka husika zizingatie usafi katika mitaro yote na wahakikishe wanaweka adhabu kali, kwa wananchi watakao kuwa wanachafua mitaro ya kupitishia maji machafu kwa makusudi kwa kutupa taka.

Pia, waweke utaratibu kwa viwanda vilivyojengwa pembezoni mwa mitaro kutunza mazingira ya ndani ya mitaro, pia kufyeka nyasi zinazoota ndani na nje ya mitaro hiyo, ili kuyaweka mazingira kuwa safi wakati wote na kuzuia maji kutwama sehemu moja.

Kila mwananchi anapaswa kuyatunza mazingira yanayomzunguka, ili kuepukana na maradhi yanayotokana na mazingira machafu.

Mikocheni ni sehemu ambazo wanakaa viongozi muhimu wa nchi, hivyo zinatakiwa kutunzwa na kuwa vizuri muda wote. Ni aibu kuwa na mazingira wanayoishi viongozi wakubwa, halafu ni machafu. Tujifunze kuyatunza mazingira, tubadili mitindo ya maisha na kuishi kwa kujali utunzaji wa mazingira katika nchi yetu.

# Kampeni ya Cha Wote ya Tigo inachochea utamaduni wa kidijitali kwa wateja (watumiaji)

**Na Mwandishi Wetu**




*Afisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha katika hafla ya uzinduzi wa kampeni ya Cha Wote.*

Leo hii malipo ya kidijitali ndiyo gumzo la mji kwa sababu yanaokoa muda, ni salama, na rahisi kwa watu binafsi na biashara. Hasa kwa biashara kwa mfano, wanatuma pesa kiurahisi kwenye akaunti zao na hata serikali sasa inaacha taratibu za kawaida za karatasi na imeanza kutumia malipo ya kidijitali si tu kwa urahisi lakini pia ili kuongeza uwazi na uaminifu katika mifumo yao.

Tigo, kampuni inayoongoza kwa mtindo wa maisha ya kidijitali nchini Tanzania, Imechukua jukumu la kuwa kiongozi katika ukuaji na maendeleo ya malipo ya kidijitali nchini Tanzania kupitia Tigo Pesa, hii ni huduma ya pesa ya simu ambayo imevuruga njia za zamani za malipo.

Baada ya kushawishi mamilioni ya wateja walioridhika ambao sasa wanatumia Tigo Pesa kwa uhuru kufanya biashara zao, Tigo hivi karibuni ilianzisha Kampeni ya Cha Wote, kampeni ya kwanza ambayo inalenga kuendeleza na kuimarisha utamaduni wa kidijitali wa kudumu miongoni mwa Watanzania.

Kampeni ya Cha Wote inajumuisha ofa za kuvutia kwa wateja wa Tigo ambao wanaweza kushinda zawadi kubwa kwa njia ya simu kwa kununua muda wa maongezi, ambapo wanaweza kushinda SMS za bure pamoja na zawadi za fedha.

Akizungumzia kampeni hiyo, Afisa Mkuu wa Tigo, Huduma za Fedha za Simu, Angelica Pesha, anasema wateja wanaweza kushinda zawadi zenye thamani ya 5,000,000/- na bonasi za dakika 100 na SMS 100 kwa siku 90.

Kwa upande mwingine, wateja wanaonunua vifurushi kwa kutumia Tigo Pesa au Tigo Rusha au kutumia Lipa Kwa Simu kulipa bidhaa na huduma kupitia programu ya Tigo Pesa wanapata nafasi ya kushinda hadi 1,000,000/- kwa siku na 5,000,000/- kwa mwezi."Kila mteja anachohitaji kufanya ili kushinda na kuongeza kipato chake ni kubonyeza Menyu ya Tigo Pesa: *150*01# au kutumia Programu ya Tigo Pesa kulipia bidhaa au huduma kupitia Lipa Kwa Simu kote nchini," Pesha anasema.

Tayari, idadi kubwa ya wateja wa Tigo Pesa wamepata zawadi kwa upande wa Kampeni ya Cha Wote. Saada Omary, muuza chakula wa Ilala, Dar es Salaam, ambaye ni mteja mwaminifu wa Tigo Pesa, sasa ananufaika na zawadi ya 1,000,000/-, anasema: "Nimetumia pesa za zawadi kuinua biashara yangu, nawashukuru sana Tigo kwa sababu biashara yangu sasa inakua kwa kasi!"

Mshindi mwingine mwenye fahari wa 1,000,000/- ni Tausi Makoba, ambaye anashangilia Kampeni ya Cha Wote akisema: "Kampeni hii imebadilisha mambo kwa sababu imegeuza maisha yangu mara moja; zawadi hii itasaidia sana kutatua majukumu yangu ya kifedha yanayonisumbua".

Pesha anaongeza kuhusu Kampeni ya Cha Wote: "Tunaamini kuwa motisha hii tuliyowapa wateja wetu itawasaidia kufikia malengo yao ya biashara kama vile kujenga nyumba, kununua viwanja, kuweka akiba kwa ajili ya siku zijazo na kukidhi mahitaji mengine muhimu ya kifedha".

Katika Kampeni ya Cha Wote, Pesha anasisitiza, 'kila mtu ni mshindi' na hivyo basi, wateja wa Tigo wanahimizwa kukumbatia huduma na bidhaa za kidijitali za Tigo na kununua vifurushi vya uchaguzi wao, iwe ni kila siku, kila wiki au kila mwezi, kwa kutumia Tigo Pesa kupitia Lipa Kwa Simu ili wasipoteze zawadi za Tigo zilizo tele.Anaongeza kuwa kampeni hiyo, inatarajiwa kunufaisha zaidi ya wateja 28,896 ambao watapata jumla ya 390ml"

Wateja wa Tigo wanahudumiwa na wafanyabiashara zaidi ya 260,000, ambao wamewekwa kimkakati kote nchini na hivyo basi, wapenzi wa Kampeni ya Cha Wote hawana haja ya kuwa na wasiwasi kuhusu wapi pa kufanya malipo ya kidijitali wanahitaji kujishindia zawadi. Wafanyabiashara kote nchini nafurahi waielekea benki, baada ya kuona ongezeko la miamala ya Lipa Kwa Simu, ambayo kwa pamoja inaongeza tofauti kubwa ya faida katika maisha.

Hili limethibitishwa na Juma Kassim wa Kassim and Sons Hardware huko Bunju, Dar es Salaam, ambaye anaamini kuwa ongezeko la faida linatokana na Kampeni ya Cha Wote, "Niligundua kuwa tangu Cha Wote ilivyozinduliwa na Tigo, wateja wamekuwa wakilipa kupitia Lipa Kwa Simu, kuna siku tulicheka kicheko cha dhihaka, wakati mteja mmoja aliposisitiza kuwa lazima alipe kwa njia ya simu malipo ya kilogramu moja ya misumari ya inchi 3 kwani hakutaka kukosa mamilioni yanayotolewa na Tigo."

Alex Massawe, mmiliki wa baa ya Utakuja Tena, ana tabasamu muda wote usoni akielezea msisimko wake juu ya jinsi anavyovuna kwa wingi kutokana na malipo ya Lipa Kwa Simu, "Niliweka hivi karibuni vituo vya Lipa Kwa Simu kwenye meza zetu, ambapo wateja wetu wanaotembelea mara kwa mara wangeweza kulipia bili zao kwa urahisi, mwanzoni walikuwa na wasiwasi, wakisema walipenda kulipa kwa pesa taslimu, lakini tangu kuzinduliwa kwa Cha Wote, wateja wetu wengi wanalipa bili zao kwa njia ya dijital kupitia Lipa Kwa Simu, wakitarajia kuwa mamilionea watarajiwa."

Kampeni ya Cha Wote inalenga kuimarisha hamu inayozidi kukua miongoni mwa wateja wa Tigo na Watanzania kwa ujumla katika kukubali utamaduni wa kidijital, hasa katika kufanya miamala - hatua inayolenga kubadilisha nchi kuwa soko lisilo na pesa taslimu katika siku zijazo.

Kulingana na Chama cha Mawasiliano ya Simu za Mkononi Duniani (GSMA) - kikundi cha viwanda kilichoko London kinachowakilisha waendeshaji wa simu za mkononi ulimwenguni kote, Tanzania kwa sasa iko miongoni mwa nchi 7 za kiongozi wa malipo yasiyo ya pesa taslimu barani Afrika. Wenzake wengine ni pamoja na Kenya, Uganda, Cote d'Ivoire, Misri, Nigeria, na Afrika Kusini.

Kwa kweli, GSMA imepongeza, katika ripoti, waendeshaji wa mitandao ya simu kama Tigo na wengine, kwa juhudi zao za kipekee katika kuonyesha uwezo wa teknolojia ya simu kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha katika masoko'.

Kwa ujumla, nchi zenye idadi kubwa zaidi ya malipo yasiyo ya pesa taslimu ni pamoja na Singapore (61%), Uholanzi (60%), Ufaransa (59%), Canada (57%), Ubelgiji (56%), na Uingereza (52%).

# Wabaini shida kupata dawa vituo vya afya

**Na Christina Mwakangale,** HANDENI

WAJUMBE wa Bodi na Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya, Halmashauri ya Mji wa Handeni, wamebainisha changamoto zilizoko katika vituo vya afya na zahanati.

Shida kubwa waliyoibaini ni upatikanaji mdogo wa dawa muhimu kulingana mahitaji hauendani na bajeti iliyotengwa.

Wamesema kila kituo kina bajeti ya dawa na vitendea kazi kutoka Bohari ya Dawa (MSD), ingawa mara nyingi upatikanaji wa dawa ni mdogo kulinganishwa na mahitaji yanayohitajika katika kituo au zahanati kwa wakati husika.

Mjumbe wa Kamati ya Zahanati ya Chanika, Halmashauri ya Mji Handeni, Fadhili Kunu, alibainisha hayo jana, alipotoa hoja na kueleza wanayokumbana nayo katika utendaji kazi wao. Ni tatizo linalosababisha zahanati au kituo kupungukiwa dawa muhimu.

Ni dosari kiutendaji zilizobainishwa wakati wa mafunzo kwa wajumbe wa Bodi na Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya, Halmashauri ya Mji wa Handeni, mkoani Tanga, yaliyoandaliwa na Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Handeni, mkoani Tanga.

"Kwa mfano, MSD imetenga bajeti ya Sh. milioni tano kwa ajili ya zahanati au kituo, Lakini utakuta dawa mnazoletewa hazilingani na bajeti hiyo.

"Labda mmeletewa dawa za Sh. milioni mbili au tatu. Je, chenji inayobaki mbona haturudishiwi hadi unakutana na msimu mwingine wa dawa?" alihoji Fadhili.

Mjumbe mwingine toka zahanati hiyo, Amri Mwenjuma, alisema suala hilo linaathiri utoaji huduma katika zahanati na vituo, hivyo uwekwe utaratibu kutoka MSD, ambao utaruhusu kituo au zahanati kununua dawa kutoka kwa mzabuni binafsi, ili kuondoa kusuasua utendaji kazi katika sekta hiyo.

"Zahanati au kituo zikiwasili dawa, vifaa vichache kutoka MSD, itolewe rukhsa palepale hiyo fedha iliyobaki MSD ikalipie dawa hata kwa mzabuni binafsi mwenye dawa ambazo tunazihitaji. Kinyume chake, jamii inaona wajumbe hatutendi kazi ipasavyo," alisema Amri.

Akijibu hoja hiyo, Kaimu Mfamasia Halmashauri ya Mji wa Handeni, Perpetua Birusya, alisema linapotokea suala hilo hufanyika ubadilishaji wa matumizi - kituo au zahanati yenye dawa za kutosha na ziada, huchukuliwa na kupelekwa kwenye mahitaji.

"Kituo, zahanati hawaitegemei asilimia 50 bajeti ya dawa kutoka MSD, na wao huchangia asilimia 50 ili ifike 100 ndipo dawa zipatikane. Ila iwapo dawa ipo nje ya hifadhi ya MSD, kinachofanyika ni mzabuni aliyeteuliwa kufuata mwongozo, ili kituo, zahanati ipatiwe dawa kwa chenji iliyobaki. Ila fedha ikishaingia MSD haitoki, utafuatwa mwongozo," alisema Perpetua.

Mtafiti kutoka DUCE, Prof. Stephen Maluka, alisema mafunzo hayo yamekuja baada ya utafiti uliofanywa na chuo hicho kubaini asilimia kubwa ya wananchi hawajui kama kuna kamati na bodi.

Prof. Maluka alisema kamati hizo, zina wajibu wa kukusanya mahitaji ya jamii, kuwasilisha kwenye timu ya uendeshaji ya zahanati na kupokea dawa kutoka MSD na kuhakikisha matumizi ni sahihi.

"Kamati ya usimamizi wa hospitali pia shughuli zake ni pamoja na kubuni vyanzo vya mapato, kuzikusanya ili kuendesha huduma, sasa kama fedha hakuna huduma zitaendeshwaje? Kamati ifanye majukumu yake, ili kuboresha huduma.

"Utafiti ulikuwa na malengo mawili makubwa; Kutathimini uelewa wa wananchi kuhusu utendaji kazi wa Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya na Bodi za Afya za Halmashauri na Kutathimini Uwajibikaji wa Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya na Bodi za Afya za Halmashauri zilizopo nchini.

"Matokeo ya utafiti yameonesha wananchi wengi hawana uelewa kuhusu kazi za Kamati na Bodi nchini. Asilimia 85.3 ya wananchi walikuwa hawajui kama kuna kamati na asilimia 96.5 walikuwa hawajui kama kuna bodi, huku asilimia 88.3 hawakuwahi kusikia kuhusu uchaguzi wa wajumbe wala kushiriki kuwachagua wajumbe," alisema Prof. Maluka.

Alisema kama wananchi hawajui kuna kamati za usimamizi, maana yake hata uwajibikaji wa kamati na bodi ni changamoto.

Alisema utafiti ulionyesha kuwa asilimia 96.7 hawajawahi kupata mrejesho wowote kutoka kwenye kamati hizo na kudhihirisha kuwa uhusiano kati ya kamati, bodi na wananchi ni mdogo.

Alieleza kuwa lengo la kufanya utafiti huo ni kuona namna kamati hizo na bodi zinaweza kuimarishwa ili zisimamie vizuri rasilimali watu na fedha kwenye vituo vya afya.

Utafiti huo ulihusisha Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya na Halmashauri ya Mji wa Handeni, mkoani Tanga. Ulifanyika kati ya Julai na Oktoba, 2022 ukishirikisha wananchi 1,184.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, akizungumza na wananchi jana, wakati akimtambulisha mkandarasi wa mradi wa maji katika Tarafa ya Naipanga, Shaban Kimaro, kutoka kampuni ya Broadway Engineering Ltd wenye gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.18, kwa lengo la kutatua kero ya maji ili kumtua mama ndoo kichwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Fedha zatajwa tatizo ufanisi ulinzi shirikishi

**Na Ester Mbilinyi,** TUDARCo

MWENYEKITI wa Mtaa wa Kajima, Kata ya Makubuli wilayani Ubungo, mkoani Dar es Salaam, Charles Kiwinza, amesema mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia fedha za ulinzi shirikishi, unawavunja moyo vijana wanaojitoa katika shughuli za ulinzi.

Kiwinza alimwambia mwandishi wa habari hizi juzi kuwa kwa sasa vitendo vya uhalifu vimepungua, lakini changamoto wanayokabiliana nayo ni mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia ulinzi shirikishi.

"Katika maeneo yangu tumeimarisha ulinzi kupitia ulinzi shirikishi, lakini changamoto ni ya baadhi ya wananchi kushindwa kuchangia fedha za ulinzi ambazo hutumika kuwalipa vijana waliojitoa kwa ajili ya ulinzi. Hali hii inakatisha tamaa vijana hawa waliojitoa kwa ajili ya ulinzi," alisema.

Kiwinza aliwaomba wananchi waendelee kutoa ushirikiano ili kuhakikisha usalama wao na mali zao unaendelea kuwapo.

Aliahidi ofisi yake kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi itaendelea kuchukua hatua dhidi ya wanaobainika kufanya vitendo vya uhalifu.

"Mtaa huu miaka ya nyuma kulikuwa na vitendo vya kihalifu kama wizi na ukabaji nyakati za usiku. Kwa sasa matukio hayo yamepungua," alisema.

Kiongozi wa ulinzi shirikishi mtaani huko, Rashim Msofe, alisema licha ya kufanya doria mtaa kwa mtaa, baadhi ya wananchi wanakwamisha jitihada zao za ulinzi kwa kutochangia ulinzi shirikishi.

Khadija Kafyome - mwenye jukumu la kuchangisha fedha kwa ajili ya ulinzi shirikishi mtaani huko, alibainisha kiwango walichojiwekea kwa mwezi ni Sh. 2,000 kwa kaya, lakini wapo baadhi ya wakazi wa mtaa huo wanakaa miezi mitatu bila kuchangia.

Aghai Kelvin, mkazi wa mtaa huo, alisema licha ya kuchangia fedha za ulinzi shirikishi, vitendo vya uhalifu vinaendelea kufanywa mtaani. Inawakatisha tamaa kuendelea kuchangia.

Jeshi la Polisi ambalo jukumu lake la msingi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, limekuwa linatilia mkazo kuwapo ulinzi shirikishi - wananchi kushiriki ulinzi katika mitaa/vijiji vyao kutokana na kuwapo idadi ndogo ya askari polisi kutosha kuyafikia maeneo yote nchini.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, katika ripoti yake ya ukaguzi maalum wa haki jinai nchini ya Machi 2021, anabainisha changamoto ya kuwapo idadi ndogo ya askari polisi, hususan askari wapelelezi. Kunakwaza utendaji wa jeshi hilo na mamlaka zingine zinazolitegemea kiutendaji, ikiwamo mahakama.

# NMB, Vodacom, Google kushirikiana kurahisisha upatikanaji wa simu janja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeanzisha ushirikiano na kampuni za Vodacom Tanzania na Google unaotarajiwa kuimarisha mapinduzi ya kidijitali kwa kuwezesha upatikanaji simu janja kwa bei nafuu nchini.

Kwa kulipa kiasi cha kuanzia cha Sh. 20,000 wateja wa Vodacom wenye vigezo watapata simu janja zinazoweza kutumia mtandao wa 4G na hivyo kuwawezesha kunufaika na fursa zinazopatikana mtandaoni.

Mpango huo mpya kwa ushirikiano wa NMB na Android (mfumo wa uendeshaji wa Google kwa vifaa vya mkononi) unakwenda sambamba na dira ya serikali ya ujumuishi wa kidijitali.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa mpango huo, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema sababu kubwa ya ushirikiano huo, ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kufikia malengo ya kidijitali yanayojenga jamii jumuishi kwa ajili ya maendeleo endelevu.

"Tunaimani kuwa mpango huu utarahisisha upatikanaji na kuongeza umiliki wa simu janja ambazo zitawasogeza zaidi wateja wa Vodacom katika ulimwengu wa kidigitali na kuanza kuchagiza uchumi wa nchi," alisema Mponzi.

Mponzi alisema kulingana na matokeo ya utafiti wa Finscope Tanzania, takribani asilimia 75 ya Watanzania wanamiliki simu ila asilimia 19 tu ndio wanaomiliki simu janja.

"Kama mnavyofahamu kuwa benki ya NMB tunayo kampeni yetu ya 'Teleza Kidijitali' ambayo inalenga kufikisha huduma rasmi za kibenki kwa Watanzania wengi zaidi. Nina imani ushirikiano huu utaongeza kasi ya kurahisisha huduma za kifedha kiganjani na hivyo kuongeza idadi ya Watanzania wanaopata huduma rasmi za kibenki," alisema.

Mkurugenzi wa Fedha wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Hilda Bujiku, wakati wa hafla hiyo alisema dhamira ya kampuni yake ni kuipeleka Tanzania kwenye ulimwengu wa kidijitali na kubadilisha maisha kupitia teknolojia.


"Ushirikiano huo unakwenda sambamba na malengo ya yetu ya kuwafungulia wateja wetu fursa zinazobadilisha maisha.

"Tunaamini kwamba ushirikiano huu utaleta mageuzi katika upatikanaji wa simu janja kwa wale ambao hawajanufaika na zana hizi za kidijitali. Vodacom imeazimia kuwezesha wateja milioni moja kumiliki simu janja zenye uwezo wa 4G katika mwaka huu wa fedha pekee, na hivyo kuchangia kupunguza pengo kati ya wanaotumia na wasiotumia intaneti nchini," alisema Bujiku.

Aliongeza kuwa mikopo ya simu ni mbinu inayowezesha umiliki wa simu janja kirahisi na kwa gharama nafuu kupitia malipo ya siku au ya wiki kwa kima kidogo cha hadi Sh. 900 huku mtumiaji akifurahia manufaa yanayokuja na kuunganishwa kidijitali. "Ushirikiano huu utatumia uwezo mpya wa kipengele cha kusimamia vifaa kwenye mfumo wa uendeshaji wa Android," alisema.

Martin Njoroge, Mkuu wa Android na Ushirikiano wa Kimajukwaa Afrika Mashariki, wakati wa hafla hiyo alisema lengo la Android ni kuwawezesha watu kupitia huduma za kikompyuta.

"Ufikiaji wa fursa zilizo kwenye intaneti ni muhimu sana kwa ukuaji wa kiuchumi na ujumuishaji wa kijamii katika nchi yoyote ile. Tunaamini kwamba ushirikiano huu utawaleta Watanzania wengi mtandaoni na kuwasaidia kutumia fursa zinazopatikana mtandaoni," alisema Njoroge.



# Utata waibuka mwananchi kujeruhiwa

**Na Jaliwason Jasson,**
SIMANJIRO

TUKIO la kupigwa na kujeruhiwa vibaya sehemu mbalimbali za mwili mkazi wa Kitongoji cha Manyara, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, Ayubu Murra, limeacha maswali mengi yasiyo na majibu.

Hali hiyo inatokana na watu wanaodaiwa kutenda uhalifu huo ni wenyeviti wa vitongoji kwenye eneo hilo.

Kwa mujibu wa chanzo chetu (jina tunalo) kuwa tukio la Murra kupigwa na viongozi hao hadi kupoteza fahamu, lilitokea Agosti 14, mwaka huu.

Mtoa taarifa huyo alisema baada ya viongozi hao kutenda uhalifu huo, mwathirika huyo alikwenda kupatiwa matibabu katika Kituo cha Afya cha Mirerani lakini Agosti 18 akiwa amelazwa yuko hoi, walifika polisi wa kituo cha Mirerani ambao walimkamata na kumweka rumande pasipo kutoa sababu zozote.

Chanzo hicho kilibainisha kuwa sababu ya kushambuliwa kwa mtu huyo ni siasa chafu zinadaiwa kuendeshwa na Diwani wa Mirerani, Salome Mnyawi, na kwamba ndiye aliyedaiwa kutoa agizo kwa wenyeviti hao kufanya uhalifu huo.

Aliyetajwa kuratibu shambulio hilo ni diwani huyo na wanaodaiwa kufanya tukio hilo ni wenyeviti wa vitongoji ambao ni, Boaz Ambonya wa Kitongoji cha Manyara na Abraham Sarakikya, wa kitongoji cha TANESCO.

"Mtu huyu alipigwa sana na wenyeviti hao, ameumizwa vibaya na aliyetoa agizo la kupigwa na kunyimwa dhamana hadi tunavyozungumza yuko rumande ni diwani wetu. Sasa nimejiuliza maswali mengi kwa nini viongozi wanachukua sheria mkononi na wanakuwa sehemu ya kutenda uhalifu?

"Hakuna sababu yoyote ya kumpiga mtu huyo ni uhuni tu wamefanya na baada ya kutendewa ubaya huo, Salome alihakikisha Murra hatoki rumande kwa kupewa dhamana na wamefanikiwa kwa hilo.alidai," kilibainisha chanzo hicho.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu kuhusu tuhuma hizo, Ambonya alisema taarifa za Murra kupigwa na wenyeviti wa vitongoji ni za uongo.

Ambonya alisema Murra anatuhumiwa kuuza ardhi ya serikali, hivyo wakati wenyeviti wa vitongoji wakifanya ukaguzi wa kufatilia vibali vya ujenzi walimkuta akiwa na mteja ambaye alimuuzia ardhi kwa Sh. 800,000 na alikuwa anataka amuuzie eneo lingine kwa Sh. 500,000.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha TANESCO, Abraham Sarakikya, alisema mtu huyo hajapigwa kosa lake ni kuuza maeneo ambayo yamezuiwa na mkuu wa wilaya katika kata ya Mirerani.

"Tulimweka chini ya ulinzi na polisi tuliwaita walikuja kumchukua na diwani hajatoa amri yoyote wala maelekezo ya kumkamata," alisema Sarakikya.

Naye Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alikiri kuwa wenyeviti hao walikuwa wanafuatilia vibali vya ujenzi.

Mwenyekiti huyo alisema inadaiwa mwathirika huyo siku hiyo alikuwa na mteja wake na hakupigwa bali alipokamatwa alijifungia chooni.

Diwani Mnyawi alikanusha tuhuma hizo kwamba hakutoa amri ya kupigwa kwa mwananchi huyo na kuongeza kuwa yuko kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na si kuwapiga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba tayari muhusika ameshafungua jalada la shambulio na kwamba wanamshikilia kwa tuhuma ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kwa kuuza viwanja vya wazi.

## Mil. 942/- kujenga na kukarabati shule

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imetoa Sh.milioni 942.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo kwenye sekta ya elimu kwa shule za sekondari katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru.

Fedha hizo zimetolewa kupitia mradi wa kuboresha elimu kwa shule za sekondari (SEQUIP) na zitatumika kutekeleza miradi hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, serikali imetoa fedha hizo kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu kwa shule za sekondari.

Alisema kuwa Sh. milioni 584.2 zitatumika kujenga shule mpya ya sekondari katika kata ya Moivo na Sh. milioni 260 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na ukarabati katika Shule ya Sekondari ya Mringa.

Mkurugenzi huyo pia alisema Sh. milioni 98 zitatumika kujenga nyumba moja ya walimu yenye sehemu ya kuishi familia mbili kwenye Shule ya Sekondari ya Kiutu.

Alisema lengo la serikali kutoa fedhahizo,ni kuboresha miundombinu ya shule za sekondari ili kupandisha kiwango cha elimu nchini.

Pia alisema dhamira ya serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo,ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanasoma katika mazingira salama ikiwamo mazingira ya kufundishia kwa walimu na kujifunzia kwa wanafunzi.

"Tunaishukuru serikali yetu,kwa kutupatia fedha hizi kwa kuwa zitakuwa na msaada mkubwa ikiwamo kukarabati na kuboresha miundombinu ya elimu kwa shule zetu za sekondari.

"Fedha hizi zitakuwa na umuhimu kwa kuwa zitasaidia kuweka mazingira mazuri na rafiki kwa walimu wakati wakifundisha na wanafunzi wakijifunza darasani," alisema.

Taarifa hiyo ilisema miradi hiyo,itatekelezwa kwa muda wa miezi mitatu kwa kutumia utaratibu uliowekwa na serikali wa kuwatumia mafundi jamii (force account).



Msongamano wa madereva wa pikipiki na bajaji wakisubiri kujaza mafuta katika kituo cha Mnyamuru wilayani Muheza mkoani Tanga jana, kutokana na uhaba wa bidhaa hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwanamume adaiwa kunyanyaswa, kujeruhiwa na mke wake wa ndoa

**Na Mwandishi Wetu,**
MOSHI

WANANCHI wa vijiji vitano vya Kata ya Mwika Kaskazini, Moshi, mkoani Kilimanjaro, wameeleza masikitiko yao jinsi serikali ilivyoshindwa kutatua sakata la mkazi wa Maring'a, Godlisten Shao, anayeshambuliwa na kujeruhiwa mwilini kwa vipigo kila baada ya muda mfupi na mkewe, ambaye anadaiwa kuwa muuzaji maarufu wa bangi na pombe haramu ya gongo.

Shao anayeishi na mkewe huyo mkabala na Shule ya Msingi Maring'a Juu (jina limehifadhiwa), anaishi kwa hofu kutokana na mkewe kudaiwa kuwatumia wateja wake kumjeruhi mumewe ili aache kiherehere cha kumfuatilia na kuripoti ukatili anaofanyiwa.

Wakizungumza jana kijijini hapo wakati wa mdahalo wa jamii unaowahusisha zaidi wanaume, kujadili nguvu na uwezo wao katika kusaidia kumaliza matatizo ya ukatili wa kijinsia katika wilaya hiyo, kwa kushirikiana na wanawake wanaharakati, wakazi hao wameitaka serikali kuacha kigugumizi cha kushughulikia malalamiko hayo.

Akizungumzia hali anayopitia kwa sasa, Shao alisema: "Nimechoka jamani nisaidieni, napigwa kila siku angalieni uso wangu ulivyo, mwili wangu umejaa majeraha (anavua shati anaonyesha tumboni na mgongoni). Naomba hata kesho polisi waje wavunje yale mabanda nimejenga mwenyewe ili mke afanya biashara halali lakini ninachovuna ni kipigo.

"Nimelalamika kwa viongozi wa serikali ngazi ya kijiji na kata, lakini nao wameshindwa. Yule mama ukimpeleka Polisi, kesho ametoka na akirudi hasira zote kwangu ananipiga. Mkuu wa Wilaya (Kisare Makori), Mkuu wa Mkoa (Nurdin Bbau), huko waliko naomba waje watusaidie, gongo na bangi iko pale kwangu."

Mkazi wa Maring'a, Lazaro Msella, alisema wanaitaka serikali kupitia ofisi ya mkuu wa wilaya ya Moshi na Jeshi la Polisi kumkamata mtuhumiwa huyo anayewasumbua na kuchukua hatua za kisheria kwa kumpeleka mahakamani, na kisha kuharibu miundombinu yote ikiwamo mabanda anayotumia kuharibu kundi kubwa la vijana na hata kuivuruga familia yake.


Aidha, Mkazi wa Mrimbo Uuwo, Simon Kawiche, ameishauri serikali kupeleka Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria, unaopendekeza kufutwa kwa adhabu ya kulipa faini kwa watuhumiwa wanaotiwa hatiani kwa makosa ya kukutwa wakizalisha au kuuza pombe haramu ya gongo na badala yake adhabu iwe kifungo peke yake ili kukomesha biashara hiyo inayoharibu maisha ya wanajamii.

Midahalo hiyo inaendeshwa na shirika lisilo la kiserikali KWIECO kwa kushirikiana na Women Fund Tanzania Trust (WFT-Trust) kupitia mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake.

Naye Reuben Shao, mkazi wa kijiji cha Lole, alisema katika kata hiyo ukatili wa kiuchumi, ubakaji, ulawiti na vipigo ni miongoni mwa matukio ya ukatili yaliyoota mizizi, huku chanzo chake kikiwa ni wanaume kutokuwajibika kwenye familia zao, na kujikita kwenye ulevi uliokithiri.

Mratibu wa mradi huo wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake, Veronica Ollomi, alisema mradi huo unalenga kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya kiakili yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani Kilimanjaro.

Aidha, alisema unalenga kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto kwa kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, inayohusiana na ukatili kwa wanawake, wasichana, watoto na makundi mengine ya pembezoni na wale walioathiriwa na vikwazo vya unyanyasaji wa kitamaduni na mijadala katika jamii za vijijini na mijini.



# Jela miaka 30 kwa kunajisi mtoto

**Na Ndalike Sonda,** ITILIMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela Omary Hussein (31) mkazi wa Kijiji cha Mwaumisheni kwa kosa la kumnajisi mtoto mwenye umri wa miaka minne.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi mahakamani hapo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Robert Kaanwa.

Hussein alishtakiwa kwa kumnajisi mtoto huyo kinyume na kifungu cha namba 130 kifungu kidogo namba 1 na 2 'e' cha sheria namba 131 kifungu kidogo namba 1 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Awali, mwendesha mashtaka wa Jamuhuri, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Jaston Mhule, aliieleza mahakama kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Julai 6, mwaka huu, katika kijiji cha Mwaumisheni.

Alidai kuwa mzazi wa mtoto huyo kufanyiwa kitendo hicho baada ya kumuogesha mtoto huyo kumwonyesha kuwa ana maumivu na baada ya kumkagua aliona ameharibiwa sehemu za siri na kuvimba. Alidai kuwa mtoto huyo alimtaja mshtakiwa na taarifa kufikishwa kituo cha polisi Itilima.

Baada ya kuwasikiliza mashahidi wanne na kielelezo kimoja kilichotolewa na upande wa mashtaka, mahakama hiyo ilimtia hatiani mshtakiwa.

Upande wa mashtaka uliomba mshtakiwa apewe adhabu kali ili iwe funzo kwake na kwa jamii kwa kuwa tukio hilo lina madhara makubwa kwa mtoto kisaikolojia na linaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

Hakimu Kaanwa baada ya kusikiliza pande zote mbili alimhukumu Hussein adhabu ya kwenda jela miaka 30.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita, akipimwa macho na mtalaamu wa vipimo vya macho, Dk. Rainphonce Kabazo (kulia), kwa kutumia kifaa cha kisasa, baada ya kuzindua kliniki ya macho ya Charity Vision Tanzania (CVT), katika Kata ya Nyasubi, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama juzi. Kushoto ni Daktari Bingwa wa macho, Josephati Boniphace. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TRA yaapa kutaifisha magari yanayojihusisha na magendo

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetangaza kiama kwa wamiliki wote wa magari yanayojihusisha na biashara ya magendo kuwa iko kwenye mpango wa kuyataifisha ikiwa ni pamoja na wale wanaotumia risiti za kughushi, hivyo kusababisha serikali kukosa mapato.

Kamishna wa Walipakodi Wakubwa wa TRA, Alfred Mregi, alisema hayo wakati wa semina ya mabadiliko mbalimbali yatokanayo na Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 kwa walipakodi wakubwa wa Kanda ya Ziwa.

"Tutashughulika na watu wanaojihusisha na biashara za magendo inayoikosesha serikali mapato. Biashara hii pia inachangia kuhatarisha afya za watumiaji na usalama wa taifa. Uingizaji wa bidhàa za magendo hapa nchini unadumaza uzalishaji kwenye viwanda vya ndani na kuleta uwiano usio sawa," alisema Mregi.

Alisema pamoja na huduma nzuri zinazowezesha watu kulipa kodi bila shuruti, bado kuna watu wanakiuka Sheria ya Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004, hivyo mzigo wa mtu yeyote utakaokamatwa ukiingizwa kwa magendo pamoja na chombo kilichohusika kusafirishia bidhaa hizo vitataifishwa.

Mregi alikemea vikali tabia ya baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wamekuwa wakitumia ankara na risiti zisizo halali ambazo zimekuwa zikibainiwa na wakaguzi wa kodi mara kwa mara jambo ambalo alidai kuwa halikubaliki kisheria.

Alisema TRA ina jukumu la kukusanya mapato ya kodi Sh. trilioni 26.7 kwa mwaka wa fedha 2023/24, hivyo mafanikio ya kukusanya kiwango hicho yanategemea michango ya walipakodi wakubwa kwa kuwasilisha kodi za marejesho na malipo sahihi.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, waliomba serikali kuhakikisha wafanyabiashara wasio waaminifu wanachukuliwa hatua kali ili kuleta usawa na ushindani ulio na tija katika uingizaji na uuzaji wa bidhaa na matumizi sahihi ya risiti na ankara.

"Hata ukikwepa kodi ni lazima kuna wakati utafika itatakiwa ukaguliwe na ukibainika umekwepa kodi kwa kipindi fulani, itakulazimu kuilipa yote tena na faini juu badala ungelipa tu mapema katika mfumo halali," alisema mfanyabiashara Godvictor Lyimo.

## Serikali yaombwa kuboresha utoaji huduma za macho

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imeombwa kuboresha kitengo cha utoaji wa huduma za macho katika hospitali za wilayani Kahama kwa kununua vifaa vya kisasa na kuwaondolea adha wagonjwa kufuata huduma hizo katika Hospitali za rufani Bugando na Muhimbili.

Inaelezwa kuwa ukosefu wa huduma hizo umekuwa ukiwasababishia wagonjwa wenye matatizo ya macho wasio na uwezo wa kugharamia safari hizo kupata ulemavu wa kudumu kutokana na gharama za matibabu kuwa kubwa.

Ombi hilo lilitolewa na mtalaamu wa macho kutoka Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dk. Deo Nyaga, wakati wa uzinduzi wa kliniki ya kisasa ya macho ya Charity Vision Tanzania (CVT) iliyoko kata ya Nyasubi.

Alisema kutokuwa na vifaa vya kisasa katika hospitali za wilaya kunasababisha huduma hiyo kuwa duni.

Dk. Nyaga alisema wamekuwa wakipokea wagonjwa wengi wenye matitizo ya macho na kuwahudumia kulingana na uwezo wa vifaa vilivyopo na wakati mwingine wanalazimika kuwapatia rufani ya Kwenda hospitali ya rufani ya mkoa, Bugando jijini Mwanza na wale wasio na uwezo wanashindwa kwenda kabisa.

Dk. Nyaga alitaja wagonjwa wanaowapokea kuwa ni wenye presha ya macho, satarani, uoni hafifu, kisukari na wengi ni wazee na kwamba uwapo wa Charity Vision Tanzania utasaidia kuwaondolea adha ya ukosefu wa matibabu ya uhakika.

Awali, Mratibu shirika lisilo la kiserikali la Charity Vision Tanzania, Mariam Mbijima, alisema tangu kuanzishwa kwa kituo hicho, wameshawafikia wagonjwa 1, 000 kati ya hao 200 wana tatizo la kuona mbali, 100 tatizo la mtoto wa jicho, 200 presha ya macho, 350 sukari na 100 wanamagonjwa mengine na wengi ni wazee.

Naye Mkurugenzi wa Kituo hicho, John Baptist, alisema tangu kuanzishwa kwa vituo hivyo nchi nzima wamewafikia wagonjwa wenye matatizo ya macho 50,000 na kwa mwezi wanapokea wagonjwa wastani wa wagonjwa 1,000 na wamefika Kahama kuwekeza baada ya kuwapo kwa tatizo hilo na wengi wanakimbilia hospitali kubwa za Bugando na Muhimbili.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya imeendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa lengo la kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu.

Mhita aliutaka uongozi wa kituo hicho kupeleka huduma pia katika halmashauri za Msalala na Ushetu.





Ukurasa 12

**Wadau wanapotaka kasi mpya Ndumbaro kutekeleza jambo lake**



Ukurasa 13

Maelekezo, maonyo ya RC kwa AZAKI zinazokengeuka



Ukurasa 14

**VITA URUSI, UKRAINE**

**Inavyomfungia nje Putin viwanja vya kimataifa, atalazimika kufuatilia mkutano BRICS kwa 'zoom'**

siasa
JUMATANO AGOSTI 23, 2023
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# Mjadala mzito wa Bandari Dar na mada za uzalendo zinavyoshindana

Na Ani Jozeni

MJADALA unaohusu ubinafsishaji Bandari ya Dar es Salaam, unakoelekea huenda umefikia kilele, bila ishara ya wazi kuwa serikali itabadili kwa kina au chochote ambacho tayari Bunge pia lilishakikubali, licha ya maelezo kuwapo makubaliano ya awali huko Dubai.

Wakati matukio ya kisiasa yenye uzito wa ziada yakijitokeza, mchakato wa urasimishaji wa mkataba huo ulikuwa umefikia pengine mbali kwa kiasi fulani.

Mabadiliko madogo ya Sheria ya Bandari kuwezesha kuingia ubia wa kiuendeshaji, si ajabu hata kubadilisha mfumo wa hisa tayari vimeshaanza kuangaliwa, ili iendeshwe kibiashara.

Mjadala huo umewakumbusha watu matukio tofauti yaliyopita, kila mchangiaji katika hadhara hii au ile, ama mitaani, kwa wale wenye umri, wakilinganisha suala hilo na mengi yaliyotangulia, ambayo mikataba yake ilitikisa taifa.

Katika medani ya siasa, kumekuwa na juhudi za kuuangalia mpango huo kama hatua iliyochukuliwa na Wazanzibari hata kuwataja Rais na Waziri, lakini hilo lilikemewa kwa nguvu kuwa si hoja ni uchonganishi au uchochezi.

Mrengo mwingine wa upinzani umekuwa na mwelekeo wa kuangalia suala hilo kama kashfa, ila halikuwa na msisitizo kwani si waziri anayehusika zaidi, ni serikali yote kwa pamoja.

Dai lingine kutoka kwenye nguzo na ngazi ya juu ya kikanisa hivi karibuni, ni kwamba Watanzania wana uwezo wa kuendesha Bandari ya Dar es Salaam.

Walichokuwa wanaashiria hapa inaelekea ni uwezo wa kitaaluma na siyo fedha za uwekezaji na kuboresha kila aina ya miundombinu ya bandari, iendane na viwango vya kimaitaifa



Msongamano forodhani, sehemu ya Bandari ya Dar es Salaam kulivyo katika uhalisi wake sasa. **PICHA: MAKTABA**

vya ufanisi,hata ikashindana na nyingine kubwa mashariki na kusini mwa Afrika.

Haina sura bayana ya kihistoria ya kampuni ya DP World ilivyokuwa na kusimamiwa, hata ikawa na ufanisi wa nchi inaoutamani.

Ukiangalia kwa karibu, unaweza kuhisi kuwa kinachobishaniwa siyo umiliki halisi wa bandari kwani suala hilo limejadiliwa kwa kirefu na kukanushwa mara kadhaa na serikali.

Kinachogomba hapo kwa kuangalia hisia za jumuiya, yaani wadau wanaokuja chini ya mwavuli wa tamko hilo, inadhaniwa ni watendaji na wasimamizi wa bandari, ambao kwa sehemu isiyo ndogo watapanguliwa na wengine wachukue nafasi zao.

Ni vigumu kusema wanahofia mishahara au kuna mengine waliyozoea ambayo yanapunguza ufanisi, kwani urasimu unaponzwa na kupenyeza rupia au pesa.

Uingiliaji huo wa suala la bandari ni kama kuzaliwa upya kwa chombo hicho katika kujaribu kumulika sera za nchi, zisiende mwelekeo wa soko na ubinafsishaji.

Kuthibitisha dhamira hiyo sheria ya uwekezaji ikaongezewa kanuni au sheria mpya, kuwa mgogoro wowote kati ya mwekezaji na serikali utatatuliwa kwa sheria za nchi, katika mahakama za ndani.

Hiyo pia imebidi irekebishwe na serikali ikachagua Mahakama za Afrika Kusini, kuwa na uwezo juu ya masuala kama hayo na DP World inawaelekeza huko hivyo ina uhakika itatendewa haki.

Waliopinga kwa nguvu mkataba huo, wanajihisi wameitingisha serikali kwa kiwango fulani, ila haielekei kuwa serikali iko mbioni kurudi nyuma.

Wakati tamko la kikanisa, linakumbushia lile la Mei 1993, hakuna picha kuwa bandarini Dar es Salaam, kutafanana na suala la umeme mwaka 2004 wakati serikali ya awamu ya tatu ilipoiweka TANESCO chini ya usimamizi wa kampuni ya Net Group Solutions ya Afrika Kusini.

Wakato huo, wafanyakazi walisimama 'ngangari' kukataa maofisa wa Net Group wasiingie ofisini, aliyekuwa Waziri wa Kazi wakati huo, akapeleka FFU kutawanya wafanyakazi hao.

Halafu wakapewa fomu ya kujiandikisha endapo mtu anataka aendelee na kazi kwa masharti ya serikali au anapingana na mwajiri. Walisalimu amri.

Kilichoko sasa, kuna mkakati wa kurekebisha kwa kina mashirika ya umma 248 na miradi kadhaa ya kushirikisha sekta binafsi inayoanza kutekelezwa muda wowote mwaka huu wa fedha.

Hizo zikienda vyema na matokeo yakaonekana, hasa kwa upande wa bandari ya Dar es Salaam, huenda wakati huo kutakuwapo lugha au kauli tofauti.

KATIBA MPYA

# Wadau wanapotaka kasi mpya Ndumbaro kutekeleza jambo lake




Katibu Mkuu wa Wizara ya Sheria na Katiba Mary Makondo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

PAMOJA na ahadi ya Waziri wa Katiba na Sheria Dk. Damas Ndumbaro, ya kuanza kuchambua mbivu na mbichi za katiba iliyopo baadhi ya wadau wanaona kama mchakato unachelewa.

Wanaharakati wa mabadiliko ya kisiasa, maridhiano na ahadi za ujio wa katiba mpya, wanaona kama masuala yanachelewa kwa vile hakuna kilichozungumzwa hadi sasa.

Wanaona muda unakwenda kwa kasi na pengine serikali ilitakiwa kufanya jambo wakati mchakato huo unapoanza mwezi ujao. Wanayasema hayo wakiangalia kuwa ni mwezi wa pili tangu kuanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 kwenye Wizara ya Katiba na Sheria.

Ni katika kikao cha mjadala unaofanyika kwa njia ya mtandao ukiandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) wa Twitter Space.

Washiriki wanaona kuwa Watanzania wengi bado hawajui umuhimu wa mchakato huo na kuonyesha wasiwasi kuwa kuna kasi ndogo ya kuanza mchakato wa kupatikana katiba mpya.

Mwezi uliopita Waziri Ndumbaro, anatangaza kuwa mchakato huo utafanywa na wasomi, asasi za kiraia, mashirika ya dini ili kubainisha mazuri na mabaya ya katiba ya sasa na kutoa mapendekezo stahiki kabla ya kuanza uandishi wa katiba mpya.

> Mchakato wa katiba mpya umegubikwa na pengo kubwa kati ya mamlaka na wananchi hivyo kuwawia vigumu watu kujua umuhimu wake, hivyo ipo haja ya kuwa na mbinu hizo.

Wakirejea vipaumbele vya Wizara Sheria na Katiba ya mwaka 2023/24, mojawapo ni kutekeleza mkakati wa kutoa elimu ya katiba kwa umma ili waweze kuelewa umuhimu wake.

Rejea ya hotuba ya Waziri Dk Damas Ndumbaro bungeni jijini Dodoma, inaweka kipaumbele hicho, huku kukiwa na kilio cha muda mrefu kuhusu madai ya katiba mpya kutoka kwa wanaharakati, wadau wa siasa za vyama vingi na wengine wanaotamani mchakato huo uanzishwe haraka.

Katika mjadala wa Twitter Space washiriki wanakumbusha kuwa Watanzania wengi bado hawajui umuhimu wa mchakato huo. Baadhi ya washiriki ni pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC Dk. Anna Henga, Rose Mwakitwange, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe Dk. Benson Bagoza, Ananilea Nkya na mwanasheria Fulgence Miku,

Wakijadili kuanza kwa mchakato wa katiba mpya, huku swali likiwa je, wananchi wamejiandaa au wameandaliwaje? Katika mchango wake Rose anasema licha ya nia njema ya serikali ya kutaka nchi ipate katiba mpya, kasi ya kufikia hatua hiyo inasubiriwa na kwamba uwekezaji katika programu ya uhamasishaji nchi nzima ni mdogo.

Mwanaharakati huyo anasema bado hajaona dhamira ya dhati ambayo itawezesha kuanza mchakato huo, huku akitamani juhudi zifanyike ili Tanzania ipate katiba mpya yenye ubora.

Kauli yake inaungwa mkono na mwanasheria Fulgence Miku, ambaye pia anasema ni muhimu kuwa na dhamira ya dhati, ili kutekeleza mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya kwa ajili ya maendeleo ya nchi, ambayo ni ahadi inayotolewa bungeni.

"Bila kuwa na dhamira ya dhati kwenye mchakato huu, inaweza kuwa vigumu kupata katiba mpya, hivyo wito wangu ni kuwapo nia na juhudi hizo ili kuhakikisia wananchi wanafikia katiba wanayotamani" anasema Miku.

MIDAHALO ZAIDI Askofu Dk Bagonza wa KKKT Dayosisi ya Karagwe anasema vikao na midahalo ya kitaifa vinahitajika ili kuwaamsha watu katika maeneo mbalimbali yanayotakiwa kuboreshwa na ujio wa katiba.

"Mchakato wa katiba mpya umegubikwa na pengo kubwa kati ya mamlaka na wananchi hivyo kuwawia vigumu watu kujua umuhimu wake, hivyo ipo haja ya kuwa na mbinu hizo," anasema Dk. Bagonza. Kwa mujibu wa Askofu huyo, Watanzania wengi hawajui umuhimu wa katiba mpya, na kwamba ni wachache wanaoifahamu, hivyo jitihada zaidi zinahitajika ili kuongeza uelewa," anasema.

"Uelewa huo utawawezesha kuwa tayari kutoa mchango chanya katika kuboresha rasimu ya katiba mpya na hatimaye waweze kupata katiba wanayoitaka kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla," anasema.

Anasema bila kuwa na vikao na midahalo ya kitaifa, mchakato wa kupata katiba mpya inayotokana na wananchi unaweza kuwa mgumu, na kwamba ni muhimu kuwaamsha ili watoe maoni yao. SIASA KIKWAZO Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga anasema kuweka mbele maslahi ya vyama kwenye mchakato wa kuandaa katiba mpya ni kikwazo, na kwamba hilo lisipewe kipaumbele.

"Kama mnakumbuka, mchakato wa mwisho wa katiba ulikwamishwa na siasa, kulikuwa na mgongano mkubwa wa kimaslahi miongoni mwa wanasiasa," anasema Dk. Anna.

Anasema kuwa kuna haja ya wadau wa mchakato wa katiba mpya kuepuka kuweka mbele maslahi ya vyama, badala yake nchi kwanza ili kusaidia kupata katiba bora ya nchi inayokubalika kwa wengi.

"Katiba mpya inapaswa kugusa wananchi kwa kuhakikisha maoni yao yanachukuliwa na kuingizwa humo kwa ajili ya maendeleo endelevu badala ya kuegemea vyama, ambavyo ni kikwazo," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji huyo wa LHRC anaongeza kuwa mchakato wa katiba hiyo uharakishwe ili ikiwezekana ipatikane haraka ili ianza kutumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka ujao.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Ananilea Nkya, anasema Watanzania wengi hawajui kuwa katiba ndiyo sheria kuu ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yao.

"Kuna haja ya kuwaelimisha waelewe umuhimu wa katiba kama ambavyo Wizara ya Katiba na Sheria iliahidi kuwa moja ya vipaumbele vyake ni kutoa kuelimisha umma kuhusu katiba," anasema Ananilea.

Ananilea ambaye pia ni Mtaalamu Mwandamizi wa Vyombo vya Habari, anasema Watanzania wasiachwe nyuma kwenye suala la katiba kwa kuwa ndio mkataba kati yao na wanaowatawala.

**MCHAKATO ULIVYO**

Mwaka 2014 mchakato wa katiba mpya ulikwama baada ya kumalizika Bunge Maalum la Katiba lililoandaa katiba pendekezwa, huku bunge hilo likiwa limesusiwa na vyama vya upinzani vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi UKAWA.

Baadaye wadau na wanasiasa wakatoa wito wa kupatikana katiba kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, lakini hawakuweza kushawishi serikali, hadi hivi karibuni ilipotangaza kuanza kwa mchakato huo.

# Maelekezo, maonyo ya RC Tanga kwa AZAKI zinazokengeuka

## • Zinapokumbushwa kodi, TAKUKURU kuzibana

**Na Mashaka Mgeta,** TANGA

MIONGONI mwa azma ya kuwepo mashirika au asasi zisizo za kiserikali (AZAKI) nchini ni kusaidia kufikisha huduma za kijamii kwa wananchi, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono mipango na jitihada zinazofanywa na serikali kwenye maeneo hayo, hivyo kuchagiza kasi ya maendeleo na ustawi wa watu.

Tofauti na mipango ya maendeleo inayotekelezwa na serikali kwa kutumia kiasi kikubwa cha fedha zinazotokana na kodi za wananchi mashirika hayo yanategemeza zaidi ufadhili wa ruzuku kutoka kwa taasisi mbalimbali za kikanda na kimataifa.

Hali hiyo, inaibua changamoto ikiwamo ya taasisi hizo kukosa nguvu za kiuchumi katika kubuni, kupanga na kutekeleza miradi inayokidhi mahitaji yaliyopo, badala yake kutegemea maeneo mahususi yanayotangaziwa ruzuku na wafadhili.

Kwa hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, anasema zipo hatua nyingi zinazopaswa kuchukuliwa na AZAKI, ili kuondokana ama kupunguza utegemezi wa ruzuku za wafadhili katika uendeshaji wa taasisi hizo.

Kindamba anatoa rai hiyo wakati akifungua mkutano wa mwaka wa jukwaa la AZAKI wenye kaulimbiu ya Mashirika yetu, Maadili yetu, Tanga yetu unaofanyika mkoani hapa.

Anasema zina mchango unaotambuliwa kwa mujibu wa sheria na kanuni, hivyo kuwa na uhalali wa kutoa huduma kutokana na uchache wa rasilimali uliopo kwenye jamii. Akizungumzia utegemezi uliopo sasa kwa AZAKI nyingi, anasema unachangia kuzifungamanisha na malengo ya wanaowapatia fedha za kutekeleza miradi wanayoitangaza, hata pale miongoni mwao inapokiuka misingi ya mila na desturi zilizopo.

Kwa mujibu wa Kindamba, wigo wa ukiukwaji wa maadili umefikia hatua kwa baadhi ya AZAKI kujiingiza kwenye kashfa za kuunga mkono, kutangaza na kushiriki vitendo viovu kama vile ushoga, ulawiti, usagaji, kuingilia kinyume cha maumbile na matumizi ya dawa za kulevya.

"Tunapitia changamoto kubwa ya mmomonyoko wa maadili kwenye jamii yetu, zipo AZAKI zinazotajwa kujihusisha na vitendo hivyo ambavyo kimsingi, ni mambo ambayo hata ibilisi hakuyafanya," anasema.

Kindamba anasema, hivi sasa jamii imeathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na kukithiri kwa mmomonyoko wa maadili unaohusisha vitendo viovu kama vile ushoga, ulawiti na usagaji.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (kulia), akikabidhi hati kwa mshiriki wa Mkutano Mkuu wa AZAKI. **PICHA: EMMA KIGOMBE**

### FEDHA CHAFU

Anaziasa zisitumike kutakatisha fedha chafu, akizionya kuwa wakati ambapo zipo katika hali duni kiuchumi na hivyo kuendelea kuwategemea wafadhili, ziepuke kutumika kama 'mirija' ya kutakatisha fedha haramu, zinazotoka kwenye mitandao ikiwemo ya ugaidi na biashara haramu za usafirishaji wa binadamu na dawa za kulevya.

> Kila DC anapaswa kuyatambua mashirika yanayofanya kazi wilayani kwake na jamii iyajue mambo yanayofanywa kwenye maeneo yao, hivyo hakikisheni mnashirikiana na serikali ipasavyo.

Mkuu wa Mkoa anaziasa kuwa na mipango yenye kuwaimarisha katika nyanja za fedha na rasilimali watu hususani wataalamu, badala ya kuwa tegemezi kwa wafadhali, wakiwamo wanaowalazimisha kujihusisha na vinavyokiuka maadili kama masharti ya kupata misaada.

Anaonya, "wakati wa uongozi wangu hapa Tanga, tutakuwa wakali sana. Hatutakuwa na simile dhidi ya vitendo vya mmomonyoko wa maadili na biashara haramu za kutakatisha fedha, kusafirisha binadamu na dawa za kulevya."

### WASHIRIKA SERIKALI

Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa AZAKI nchini, Mwantumu Mahiza, anasema taasisi hizo zinapaswa kufuata sheria, kanuni na taratibu ili kujiimarisha zaidi na kuepuka kufutiwa usajili.

Aidha, miongoni mwa matakwa ya kisheria ni kulipa kodi zinazotambulika na mamlaka za serikali hususani ofisi za Wakuu wa Wilaya wanapotekeleza miradi yao.

"Kila DC anapaswa kuyatambua mashirika yanayofanya kazi wilayani kwake na jamii iyajue mambo yanayofanywa kwenye maeneo yao, hivyo hakikisheni mnashirikiana na serikali ipasavyo," anasema.

### TAKUKURU KUCHUNGUZA

Kuhusu kodi, anasema uchunguzi uliofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kudhibiti Rushwa (TAKUKURU) unabaini kuwapo AZAKI zinazokwepa kodi.

Hata hivyo, anasema mpango umeandaliwa ili kuziwezesha kujua kwa kina maeneo mahususi ambayo TAKUKURU inazichunguza taasisi hizo, hali itakayoondoa mtazamo na hisia hasi zinazoweza kujitokeza.

Mwantumu anasema huduma za AZAKI zinapaswa kuelekezwa zaidi katika kero kubwa zinazowakabili wananchi kama migogoro ya ardhi na msaada wa kisheria hasa kwa watu wanaokabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Hata hivyo, Mwantumu anaonya kuwa zipo zinazotekeleza majukumu yasiyoendana na malengo yaliyoanishwa kwenye katiba zao na kuzionya kuwa jambo hilo halikubaliki.

Anasema serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu utendaji kazi kujiridhisha kuwa zinafuata misingi ya ukweli na uwazi.

Kadhalika, ufuatiliaji shughuli na uendeshaji wake ufanywe kwa njia ya mfumo, hivyo kuondoa dhana kwamba inafanywa na mtu binafsi.

Anaziasa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, ili kufikia malengo ya kuisaidia serikali kupata suluhu ya kero zilizopo kwenye jamii na siyo kujinufaisha binafsi.

Mwantumu aliyewahi kushika nyadhifa tofauti za uongozi serikalini na ubunge, anasema ili kuboresha utengamano miongoni mwa taasisi hizo, uongozi wake ulianzisha mfumo wa kuwepo majukwaa ya taasisi hizo kuanzia ngazi za chini kwenye jamii hadi kitaifa.

"Zamani majukwaa ya AZAKI yalifanyika ngazi ya kitaifa, lakini niliagiza yaanzie kwenye ngazi za chini katika jamii. Ndio maana hata leo mnaofanya kazi wilayani mnajuana, na kushirikiana kwa kina tofauti na ilivyokuwa awali,"akasema.

### KUWASILISHA TAARIFA

Katibu Tawala wa Mkoa, Pili Mnyema anaziagiza kuwasilisha taarifa zao serikalini ili kufanikisha azma ya utaratibu na usimamizi wa shughuli zao, kwa mujibu wa sheria.

"Hatuwezi kuwasimamia na kuwaratibu kama hatuwafahamu. Bila sisi kuwajua, itakuwa vigumu kutoa huduma mnapohitaji. Hivyo timizeni wajibu wa kisheria kuwasilisha taarifa zenu kwa ukweli na uwazi," anasema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la AZAKI (NACONGO), Miraji Malinda, anasema pamoja na ufanisi wake, taasisi hizo zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ukiwemo mtazamo hasi kwenye jamii kwamba wana fedha zinazoweza kutumika hata kinyume cha utaratibu.

Aidha, anasema ipo haja kwa AZAKI za kikanda na kimataifa zinazofika kwenye maeneo yao kufanya kazi, yakajitambulisha kwenye baraza katika ngazi husika, ili kuweka kumbukumbu na rekodi zinazojulikana kwa serikali na NACONGO.

***Mwandishi ni Ofisa Habari Mkuu Mkoa wa Tanga.***
***Mawasiliano: 0754 691540, email mgeta2000@yahoo.com***

VITA URUSI, UKRAINE

# Inavyomfungia Putin kimataifa, atafuatilia BRICS kwa 'zoom'

Na Gaudensia Mngumi

• Licha kutoshiriki wajumbe waikubali, kuitetea Moscow



Baadhi ya marais wa BRICS, kushoto ni Xi Jinping wa China, Vladimir Putin, Urusi na Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini (kulia). **PICHA: AFP**

JULAI mwaka huu Afrika Kusini ilimpiga marufuku Rais wa Urusi, Vladimir Putin, kuonekana nchini humo kwenye mkutano wa kilele wa mataifa yanayoinukia kiuchumi maarufu BRICS.

Kikao hicho cha wakuu kinafanyika Johannesburg kuanzia jana hadi kesho kikiwaleta wanachama wa kundi hilo ambao ni Brazil, India, China na Afrika Kusini, wanaoshirikiana kwenye maeneo mbalimbali kuanzia uchumi, teknolojia hadi diplomasia.

Tangazo hilo lilimaliza uvumi wa miezi kadhaa kuhusu iwapo nchi hiyo ingemkaribisha Putin ili kumkamata kwa hati ya kimataifa, kiongozi huyo anayetuhumiwa kuivamia Ukraine.

Afrika Kusini ilikabiliwa na mkanganyiko katika kuandaa mkutano huo kwa sababu, kama mwanachama wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), chombo hicho kilitoa hati ya kumkamata Rais Pitin, kwa mujibu wa Reuters.

Hati ikitolewa Machi 2023, Afrika Kusini ingelazimika kumkamata Putin kwa madai ya uhalifu wa kivita unaofanywa na Urusi kwa kuivamia Ukraine.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi, Sergei Lavrov, ndiye anayeiwakilisha nchi hiyo kwenye mkutano huo wa kilele wa BRICKS Johannesburg , Agosti 22-24 badala ya Putin, inasema Reuters..

Kufungiwa nje Putin kulifuatia mazungumzo kati ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa na viongozi wa vyama vya siasa kutoka kundi la nchi zinazoinukia kiuchumi BRICS kuangalia uwezekano wa kumweka kando asije kunasa nyavu za ICC.

Ikulu ya Kremlin wakati huo ilisema Putin atashiriki kwenye mkutano wa kilele wa BRICS kwa njia ya video.

### UMUHIMU WA BRICS

Licha ya Putin kubaki nyumbani mataifa hayo ni muhimu kwa Moscow, kwani ni kama sehemu yake ya kujiegemeza. Kwa Urusi, mkutano wa kilele wa BRICS ni muhimu mno. Kwanza ni fursa ya kuonyesha kwamba haihitaji tena nchi za magharibi kufuatia jitihada za kuitenga Moscow katika jukwaa la dunia kutokana na vita vyake huko Ukraine.S

BRICS ni kama jukwaa muhimu la kuikosoa Marekani na kwa njia nyingine mdomo wa kuisema Urusi kutoka na kukandamizwa na nchi za magharibi zikiongozwa na Marekani.

Kwa hiyo mtandao wa jarida la The Conversation Africa Edition, unaofuatilia mkutano huo Afrika Kusini unasema:" Wakati viongozi wa kundi la BRICS ambalo lina mataifa makubwa kiuchumi yanayoinukia - Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini, wanapokutana Johannesburg kwa siku mbili kuanzia jana, watunga sera za kigeni

> Tunapaswa kuendeleza utaratibu wa kidemokrasia zaidi wa kidunia kwa kuhakikisha ushiriki kamili wa nchi zinazoendelea katika vyombo vya maamuzi.



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky



Rais wa Urusi, Vladimir Putin

huko Washington Marekani bila shaka watakuwa wakisikiliza kwa makini kinachoendelea."

Unaongeza kuwa kundi la BRICS limekuwa likipinga baadhi ya kanuni muhimu za uongozi wa kusimamia mataifa mengine wa Marekani katika miaka ya hivi karibuni.

Kwa upande wa kidiplomasia, imedhoofisha mkakati wa Ikulu ya White House kuhusu Ukraine kwa kuyakabili maelekezo ya kutumia vikwazo dhidi ya Urusi.

Aidha, kiuchumi, imejaribu kuibana Marekani kwa kuondokana na kuienzi sarafu yao kwa kudhoofisha matumizi jukumu la Dola kama sarafu kuu na ya msingi duniani.

### KUONGEZA NGUVU

Na sasa kundi hilo linaangalia kupanuka na kuongeza wanachama rasmi hadi wafike 23, hatua kama hiyo ikiwa BRICS ikiziangalia Iran, Cuba au Venezuela mataifa ambayo yataimarisha upinzani wa kundi hilo dhidi ya Marekani.

Leo Zipo Brazili, Russia, India, China na Afrika Kusini.

Nchi za BRICS zinaungana karibu ili kusimamia maslahi ya pamoja ya maendeleo na jitihada za mpangilio wa kuhakikisha dunia inashikamana kwa pande nyingi siyo kuwa chini ya taifa moja lenye nguvu ili kuepusha kuwa na mbabe mwenye mamlaka anayotawala wote.

Hata hivyo, kuimarika kwa BRICS kunaligeuza kundi hilo kuwa na nguvu ya mazungumzo yenye uzito ambayo sasa inapinga malengo ya kisiasa na kiuchumi ya Washington, linakuwa kama kitu kizito kinachoigonga Marekani kichwani.

Kwa hiyo zama za kuipuuza BRICS kama nguvu kuu ni jambo ambalo Marekani haitalifanya na sasa ni kuwa na mwelekeo wa pengine wa kujijenga upaya, unashauri mtandao wa The Conversation.

### KULETA MAPYA

Mwanzoni mwa ushirikiano wa BRIC mwaka 2008, kabla ya Afrika Kusini kujiunga mwaka 2010 na kuongeza "S" kutoka kwenye BRIC- wanachama waliamini kuwa kuwapo kwa kundi hilo kunaweza kusababisha mvutano na watunga sera ambao waliiona Marekani kama "taifa muhimu na la lazima duniani."

Kama Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani wa Brazili, Celso Amorim, alivyosema wakati huo, "Tunapaswa kuendeleza utaratibu wa kidemokrasia zaidi wa kidunia kwa kuhakikisha ushiriki kamili wa nchi zinazoendelea katika vyombo vya maamuzi."

Kwake BRIC ni kama daraja kati ya nchi zilizoendelea kiviwanda na zinazoendelea ili kupata maendeleo endelevu na sera ya uchumi ya kimataifa yenye uwiano na ulinganifu isiyowaache wengine nje.





# Mikoa 10 hatari uharibifu ardhi yatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja mikoa 10 inayokabiliwa na uharibifu mkubwa wa ardhi huku ikibainisha mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo aliitaja mikoa hiyo jijini hapa jana alipowasilisha taarifa kuhusu hatua zilizofikiwa katika kuhuisha Sheria ya Mazingira (2004) na ya Hali ya Mazingira (2021-2023) kwa Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Aliitaja mikoa yenye uharibifu mkubwa wa ardhi ni: Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Lindi, Pwani, Simiyu, Manyara, Arusha na Ruvuma.

Kukabiliana na tatizo la uharibifu wa ardhi ulioathiri baadhi ya maeneo nchini, alisema Jafo serikali kwa kushirikiana na wadau imeanza kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo usimamizi endelevu wa hifadhi ya ardhi katika mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga, Tabora na Bonde za Ziwa Nyasa.

Dk. Jafo alitaja miradi hiyo ni pamoja na wa usimamizi endelevu wa mifumo-ikolojia ya miombo magharibi mwa Tanzania, usimamizi wa ardhi ya Kilombero na Rukwa na usimamizi endelevu wa mfumo ikolojia ya Mlima Kilimanjaro.

Alisema serikali imewezesha uandaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 2,556 kati ya vijiji 12,318 unaosaidia wananchi kupanga namna sahihi ya matumizi ya ardhi bila kuathiri mazingira.

Alisema uharibifu wa ardhi kwa kiasi kikubwa husababishwa na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu zinazosababisha kuondolewa uoto wa asili, upotevu wa udongo na ubora wa udongo.

Pia alisema, shughuli hizo zinajumuisha kilimo kisicho endelevu, ufugaji wa mifugo usiowiana na maeneo ya malisho, shughuli zisizo endelevu za uchimbaji madini na uchomaji moto ovyo.

Dk. Jafo alitaja tatizo lingine ni kuenea viumbe vamizi na ukataji miti ovyo kwa ajili ya mbao, kuni na ujenzi ambavyo huchangia kwa kiasi kikubwa kuondoshwa uoto wa asili.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21, mbali na mambo mengine, imebainisha kuwapo dosari ya matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi, ikiwamo Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA) huku mamlaka za hifadhi zikiwa hazina vifaa vya kisasa wala mafunzo ya kukabiliana na matukio hayo.



Naibu Waziri wa Madini, Dk. Stephen Kiruswa (wa tatu kulia), akikata utepe kuzindua maonyesho ya madini na fursa za uwekezaji, Mjini Ruangwa mkoani Lindi juzi. Wa pili kulia ni Mkuu wa Mkoa huo, Zainab Tellak. **PICHA: GIFT THADEY**

## Idara ya Tathmini na TAKUKURU zakumbusha mfumo wa utendaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, ameagiza Idara ya Ufuatiliaji na Tathimini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kutumia mfumo wa kitaifa ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aliagiza hayo jana katika kikao kazi cha mapitio kilichohusisha wakurugenzi wa idara na wakuu wa vitengo wa ofisi hiyo, Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ikiwasilisha Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Shughuli za Kiserikali.

Alisema eneo la ufuatiliaji na tathmini haliwezi kukwepeka na mfumo huo utasaidia kushauri namna ya kujipanga na jinsi ya kufanya kazi ndani ya serikali na kuchakata kila kitu ili kupata matokeo sahihi katika kupima utendaji kazi.

Waziri huyo alisema kuwa kwa mujibu wa sheria, kuna taasisi ambazo zimekasimiwa majukumu ya kufanya, zinazofanana na idara hiyo ikiwamo Tume ya Taifa ya Mipango.

"Ni lazima kufanya tathmini na ufuatiliaji wa matumizi sahihi ya fedha katika utekelezaji wa miradi na utendaji wa shughuli za serikali, eneo hili kwenye mfumo liwekwe vizuri na liweze kutusaidia," aliagiza.

Naibu Waziri wa ofisi hiyo, Ummy Nderiananga, alisema wasilisho la mfumo huo linatoa mwelekeo wa utendaji wa shughuli za serikali utakaosaidia Ofisi ya Waziri Mkuu kuratibu vizuri shughuli zake.

Mkurugenzi wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali wa ofisi hiyo, Sakina Mwinyimkuu alisema idara yake itajitahidi kufuatilia kwa ukaribu ukamilishwaji wa mfumo huo kwa wakati.

Awali, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa ofisi hiyo, Innocent Mboya, alisema amepokea maelekezo ya kukamilisha mfumo huo ndani ya mwaka huu wa fedha (2023/24).

"Tunaahidi kwamba ndani ya hizi wiki mbili, tutakuwa tumeandaa mpango kazi ambao utatupeleka kwenye ramani na utekelezaji wa mfumo huu, na ndani ya miezi mitatu tutakuwa tumekamilisha mfumo huu kwa kufuata matakwa na maelekezo ya serikali," aliahidi.

## Ukifanya ununuzi wa umma nje ya mfumo wa NeSt umetenda jinai

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya umma itakayobainika kufanya ununuzi bila kutumia mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma (NeST ), itakuwa imetenda kosa la jinai.

Mfumo huo umeundwa na Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (PPRA) ili kuondokana na upungufu uliojitokeza katika mfumo wa awali wa TANEPS.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Victorina Ludovick, akimwakilisha Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Fatuma Mganga, alitoa angalizo hilo jana wakati wa mafunzo kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka halmashauri zote za mkoa huo.

Alisema serikali inazitaka taasisi zake kutumia mfumo huo, hivyo michakato yote ya kufanya ununuzi wa umma serikalini, ni lazima ifanywe kupitia mfumo wa NeST.

Ludovick alisema mfumo huo utaleta uwazi zaidi katika taratibu za ununuzi na kuongeza tija katika shughuli za serikali, hasa kwenye fedha ambazo sehemu kubwa ipo kwenye ununuzi. Asilimia 80 ya bajeti ya serikali imekuwa ikielekezwa katika ununuzi.

Mkuu wa Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi Sekretarieti ya Mkoa wa Singida, Nkuli Nketo, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutumia mfumo huo mpya kuanzia Oktoba Mosi mwaka huu.

"Baada ya mafunzo haya, watumishi wa halmashauri wataweza kutumia mfumo huo na ifikapo Septemba 15 mwaka huu, watakuwa wameandaa mipango ya ununuzi kwenye halmashauri zao na kuwasilisha katika mfumo wa NeST," alisema.

Nketo alisema mfumo umeanzishwa ili kufanya mabadiliko kutoka kwenye mfumo wa awali wa TANePS ambao ulionekana baadhi ya taasisi zilishindwa kuutumia, lakini sasa mfumo wa NeST umeboreshwa zaidi na umepunguza mlolongo mrefu wa kufanya ununuzi.

## Jaji Kiongozi Uganda asifu Kituo Jumuishi utoaji haki Tanzania

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu Uganda, Dk. Flavian Zeija, ameipongeza Tanzania kwa kuwa na Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki kinachosaidia kupunguza gharama kwa wananchi wanaokwenda kutafuta haki zao za msingi mahakamani.

Dk. Zeija alitoa pongezi hizo jana alipotembelea Makao Makuu ya Mahakama Tanzania jijini hapa pamoja na Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki.

Dk. Zeija alisema kuwapo kwa kituo hicho chenye huduma zote sehemu moja, kunarahisisha watoaji haki kufanya kazi zao na kuwapunguzia gharama watafutaji haki.

"Ninawapongeza sana kwa ubunifu huu, ni mfano mzuri wa kuigwa. Baadhi ya miundombinu na maeneo ikiwamo ofisi za viongozi na watumishi wa mahakama katika jengo hili nimejifunza mengi ya kuiga katika ziara hii," alisema Dk. Zeija.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alimshukuru jaji huyo kwa kuwatembelea, akisema ujio wake ni faraja kwa watumishi na utachangia kuongeza jitihada za kiutendaji wa kila siku.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma, Dk. Juliana Massabo, alisema ndani ya kituo hicho kuna Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Watoto, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na masjala ndogo ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania.



HABARI MBEYA

# Madaktari bingwa waweka kambi tiba ya macho

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADAKTARI bingwa wa macho kutoka Ujerumani wameungana na madaktari wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya kuendesha kambi ya matibabu ya macho kwa wananchi kutoka maeneo mbalimbali.

Kambi hiyo ilizinduliwa jana na Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ambaye ni miongoni mwa wawezeshaji wa jambo hilo akishirikiana na uongozi wa hospitali hiyo.

Akizungumza wakati wa kuzindua kambi hiyo, Mahundi alisema aliamua kushirikiana na hospitali hiyo kuwezesha matibabu hayo baada ya kubaini kuwa watu wengi wana matatizo ya macho lakini hawana uwezo wa kugharimia matibabu. Mahundi alisema amekuwa na utaratibu wa kusaidia makundi mbalimbali ya jamii lakini safari hii aliwiwa kuhudumia watu wenye matatizo ya macho ambayo yamekuwa yakiwagharimu wananchi fedha nyingi.

"Tulianza kwa kuwasaidia wanawake wenye tatizo la fistula ambalo huwa linawafedhehesha, baadaye tuliamua kuwasaidia wenye matatizo ya macho ambayo pia ni gharama kubwa kwa mwananchi mmoja mmoja," alisema Mahundi.

Alisema baadhi ya huduma za macho wananchi wamekuwa wakilazimika kusafiri umbali mrefu kwenda kuzifuata Dar es salaam.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Abdalah Mmbaga, alisema huduma zitakazotolewa katika kambi hiyo ni pamoja na upimaji wa macho, utoaji wa dawa na upasuaji wa mtoto wa jicho kwa wenye tatizo hilo.

Alisema gharama za matibabu ya macho hasa upasuaji ni Dola 90 za Marekani sawa na Sh. 220,000 ambazo alisema asilimia kubwa ya wananchi wa kawaida hawana uwezo wa kumudu kulipa wanapotaka kufanyiwa matibabu hayo.

Katika kambi hiyo inayoendelea katika hospitali hiyo, alisema matibabu yote yatagharamiwa na madaktari wa Ujerumani ambao wanatoka kwenye taasisi moja isiyo ya serikali ya nchini humo.

"Huduma hizi tulipanga kuanza leo (jana) mpaka Agosti 29 lakini kutokana na watu wengi kuanza kujitokeza tangu jana (juzi) tuliamua kuendelea ambapo tuliwahudumia zaidi ya watu 30 ambao wanane kati yao walibainika kuwa na mtoto wa jicho na wanne tayari wamefanyiwa upasuaji," alisema Dk. Mmbaga.

Aliwapongeza wananchi kwa kujitokeza kwa wingi kwenye matibabu hayo kwa kuwa ni fursa kwao kutokana na kwamba gharama za matibabu hayo ingekuwa kubwa endapo wangetumia fedha zao.

Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali hiyo, Dk. Frolian Kaijage, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi kutokana na hospitali hiyo kwa sasa kuwa na miundombinu bora ya utoaji wa huduma.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwapongeza wadau wote waliojitolea kuwahudumia wananchi. Alisema huduma hiyo itasaidia kutatua matatizo yanayowakabili wananchi.

Mbeya imebainika kuwa miongoni mwa mikoa yenye idadi kubwa ya wananchi wenye matatizo mbalimbali ya macho hasa mtoto jicho na taasisi mbalimbali zimeanza kusaidia matibabu kutolewa bure.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, akizungumza na wananchi waliojitokeza kupata matibabu ya macho katika kambi maalumu inayoendeshwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa macho kutoka nchini Ujerumani, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Dc acharuka kuibuka kwa mauaji, ubakaji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, amewataka wananchi wilayani hapa kuacha kufanya matukio ya mauaji na ubakaji kwasababu yanazidi kuchafua wilaya hiyo.

Kasongwa aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujio wa tamasha la pili la utamaduni kitaifa litakalofanyika viwanja vya sabasaba mjini hapa.

"Pia matukio ya kutisha kama mauaji, ubakaji kipindi hiki ambacho wageni wapo tunaomba matukio hayo myaache kwa sababu yanazidi kutuchafua. Kila siku matukio ya ajabu Njombe si kwamba tunasapoti wageni wakiondoka mwendelee hapana na kipindi hiki mwendelee kuwa na tabia njema nzuri," alisema.

Mkuu wa wilaya alisema tamasha hilo linatoa fursa kwa Watanzania kusherehekea utajiri na urithi wa utamaduni na kuwahamasisha wananchi wapende kuhifadhi, kulinda na kuendeleza mila ambazo ndio msingi wa maadili na utambulisho wa taifa.

Pia alisema kutakuwa na maonyesho ya kazi mbalimbali za kitamaduni na mashindano ya ngoma na vyakula vya asili vya kikanda.

Mkurungenzi Idara ya Utamaduni kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Mnata Resani, alisema tamasha hilo baada ya kufanyika kwa mara ya kwanza jijini Dar es Salaam hivi sasa litafanyika Njombe kuanzia Agosti 25 hadi 27, mwaka huu.

"Tunaleta zaidi ya watu 2,000 kutoka nje ya Njombe watafika hapa. Wawe machifu, wasanii kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania watahitaji kula, kuvaa na mahitaji yote watapata kutoka kwa wenyeji," alisema Dk. Resani.

# Wataka Rais Samia kutoyumbishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MJADALA wa Mkataba wa uwekezaji wa bandari kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya DP World ya Dubai, umeendelea kushika kasi mkoani Mbeya huku baadhi ya viongozi wa dini wakimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutoyumbishwa na kelele.

Jana, Kiongozi Mkuu wa Kanisa la Gospel Miracle Church for All People (GMCL), Nabii David Mpanji, alisema lengo la serikali kualika wawekezaji kwenye bandari ni kutaka kuongeza ufanisi kwenye uendeshaji na kupunguza muda wa mizigo kukaa bandarini.

Alisema endapo uwekezaji huo utafanikiwa kuna uwezekano wa bidhaa mbalimbali ambazo zinaingia nchini kupitia bandari hiyo kushuka bei na hivyo wananchi kupata unafuu wa maisha.

Alimshauri Rais Samia kuendelea kuwa imara kwa kuhakikisha anafanya kile ambacho anaamini kuwa kinafaa kwa maendeleo ya taifa na kwamba kinachoendelea kwa uelewa wake si kuuza bandari kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakidhani.

Hata hivyo, alisema watu na taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikitoa matamko ya kupinga uwekezaji huo yawezekana hayajui faida za mradi huo na hivyo akawataka kuwasikiliza wataalamu.

"Lakini pia nchi yetu inaendeshwa na misingi ya katiba na sheria. Wako Watanzania ambao wanadini na wasiokuwa na dini, kila mtu akiamua kutoa matamko tutalivuruga taifa letu na mimi naamini kwamba hao wanaotuvuruga ni madalali," alisema.

Nabi Mpanji aliwataka Watanzania wanaomkosoa au kumshauri Rais wafanye hivyo kwa busara kwa kuwa ndiye kiongozi mkuu wa nchi.

Kutokana na malumbano yanayoendelea nchini, alisema kuna hatari ya mpasuko kutokea, hivyo kusababisha amani iliyopo kuvunjika jambo ambalo alisema halitakuwa na afya kwa taifa.

Alisema wako wapotoshaji ambao wanawalazimisha Watanzania kuamini kwamba mkataba wa bandari ni mbaya jambo ambalo alisema siyo sahihi.

Alisema baadhi ya wanaopinga wanapigania maslahi yao binafsi na baadhi yao wanatumika kama madalali wa kupigania maslahi ya watu wengine.

"Kila mtanzania anatakiwa kuhakikisha analinda amani ya nchi pamoja na kumwombea Rais Samia na viongozi wengine wa serikali ili waendelee kuliongoza taifa kwenye misingi inayotakiwa," alisema.





## Mita za malipo ya kabla kuongeza usambazaji maji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara, amesema mita za malipo ya kabla ni miongoni mwa mbinu zitakazowezesha ukusanyaji wa mapato na usambazaji maji.

Aliyasema hayo jana mjini Zanzibar alipofungua kikao kazi na mafunzo kwa wakurugenzi wa huduma kwa wateja wa mamlaka ya maji za Tanzania.

Alisema mita hizo zitapunguza malalamiko ya malipo kwa wateja na kuziwezesha taasisi kupata mapato kwa wakati, hivyo aliwataka watoa huduma kutoa huduma bora kwa wateja na sio kuwakandamiza.

Kaduara alisema wananchi na wateja wa mamlaka za maji wana wajibu kuhakikisha wanalipa bili zao za maji kwa wakati kwa kuwa mfumo wa sasa unaotumika unamfanya mteja kuhakiki mita zao kabla ya bili kutoka.

Alisema mafunzo hayo yatachangia kuboresha ufanisi wa huduma wanazozitoa na kuwezesha wananchi kupata huduma bora ya majisafi na usafi wa mazingira.

Alisema mamlaka za maji zina jukumu kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uwiano na ubora unaotakiwa.

"Ninafahamu kuwa mada kuu ya mafunzo haya inajikita katika maeneo kadhaa ambayo yataongoza safari yetu ya kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya maji nchini," alisema.

Akizungumzia udhibiti wa madeni, waziri huyo alisema ni changamoto inayohitaji mikakati thabiti wa kuidhibiti na kutafuta mbinu za kisasa katika makusanyo na kuweka mwelekeo mzuri wa kifedha ili mapato kukusanywa kwa ufanisi zaidi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Balozi Issa Suleiman, alisema tangu nchi ipate uhuru, kuna tatizo la maji kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuongezeka idadi ya watu na mahitaji.

Alisema uchumi unapokua na maji yanahitajika kwa wingi, hivyo serikali imejipanga kutoa huduma hiyo kwa wateja kadri wanavyoongezeka.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Zanzibar imepiga hatua na kufikia asilimia 66 ya upatikanaji wa maji, hivyo kazi kubwa imefanywa na watalamu wa maji na kusimamiwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Maji mkoani Tabora, Biswalo Bernard, alisema huduma ya maji ni muhimu kwa wananchi, hivyo unahitajika weledi katika kutoa huduma kwa wananchi.

# Waziri ashtukia mkakati serikali kupingwa uwekezaji bandarini

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hamza Hassan Juma, amesema sera ya ubinafsishwaji mashirika ya umma na viwanda imekuwapo tangu enzi za serikali ya awamu ya tatu, hivyo anashangaa wanaompinga Rais Samia Suluhu Hassan kukaribisha uwekezaji wa Kampuni ya DP World bandarini.

Alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Vuga, mjini Zanzibar, kufuatia mjadala unaoendelea wa uendelezaji bandari ambao umewagawa wananchi na viongozi wa madhehebu ya dini nchini.

Alisema kimsingi, Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa ndiye aliyeasisi sera ya ubinafsishwaji wa mashirika ya umma na viongozi waliomfuatia waliendeleza mpango huo akiwamo Rais Jakaya Kikwete.

Hata hivyo, kitabu chake cha My Life My Purpose (Kusudio la Maisha Yangu), Mkapa anautaja uamuzi wa kubinafsisha mashirika ya umma kuwa miongoni mwa mambo anayojutia.

"Katika miaka ya nyuma, tulishughudia Shirika la Ndege likibinafsishwa, huduma za kibenki na viwanda na katika mpango huo kuna maeneo yalifanikiwa na kuna maeneo hayajafanikiwa kama vile huduma za usafiri wa anga pamoja na usafiri wa reli," alifafanua Hamza.

Waziri huyo alisema serikali awamu ya tano chini ya Rais Jakaya Kikwete ilibinafsisha huduma za gesi kupitia bomba la gesi kutoka Mtwara kwa kampuni ya nje ya nchi na hakuna mtu aliyejitokeza kulalamika na kupinga kwa sababu ni mpango uliolenga kuimarisha upatikanaji huduma hiyo.

Hamza alisema chini ya uongozi wa Rais Samia, serikali imeonesha mwelekeo mzuri katika kuimarisha demokrasia na diplomasia ya Tanzania na mataifa mengine, mambo ambayo yalitetereka katika siku za nyuma.

Alikumbusha kuwa Rais Samia baada ya kushika wadhifa alionao sasa, aliwaachia mashekhe waliokuwa kizuizini, wakikabiliwa na kesi ya ugaidi, wanasiasa waliokuwa wakikabiliana na kesi akiwamo Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na kuwataka wanasiasa waliokuwa wamekimbia nje ya nchi kurejea nchini na kuhakikishiwa usalama wao, akiwamo Tundu Lissu.

"Tundu Lissu na (Godbless) Lema walikimbilia nje ya nchi, lakini juhudi za Mama Samia za kujenga demokrasia na misingi ya utawala bora, zimewafanya warejee na kuendelea na harakati za kisiasa. Leo wanapita na kuanza kumshambulia bila kukumbuka wema wake," alisema.

Waziri Hamza alisema kuwa vyama vya upinzani kwa zaidi ya miaka saba havikufanya mikutano ya hadhara mbali na wabunge na wawakilishi ambao waliruhusiwa kufanya mikutano katika majimbo yao chini ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Pia alizungumzia tamko la kupinga mkataba wa uendelezaji huduma za bandari lililotolewa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), akisema wakati umefika viongozi wa dini wafanye kazi za dini na viongozi wa kisiasa wafanye kazi za kisiasa badala ya kuchanganya mambo na kusahau majukumu yao.

Alisema kinachoonekana sasa mjadala wa mkataba wa bandari umelenga kumtia doa Rais Samia kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 baada ya kuona amepata mafanikio makubwa katika uongozi wake.

Waziri huyo alisema kila mmoja ameshuhudia uwezo wake katika kuendeleza miradi iliyoachwa na mtangulizi wake ikiwamo ya kuzalisha umeme, reli ya kisasa na kujenga vituo vya afya katika mikoa mbalimbali ili kuimarisha huduma za tiba nchini.

Pia alisema kuwa kama kuna mwanachama yeyote wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) anapanga kujitokeza kumpinga Rais Samia katika Uchaguzi Mkuu ujao, "watammaliza ndani ya chama" kwa vile ni kinyume cha utaratibu wao.

Alidai kuna watu wanataka kufifisha mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wa Rais Samia, wakitumia silaha yao kubwa - Mkataba wa Bandari kuwapotosha wananchi kwa maslahi yao binafsi ya kisiasa kuekelea 2025.

Waziri huyo alisema ni jambo la kushangaza watu wameacha kujadili mambo ya msingi, zikiwamo huduma za kijamii na kiuchumi zinazoimarishwa, badala yake ajenda kubwa imekuwa Mkataba wa Bandari na kukaribisha siasa za ubaguzi katika mfumo wa Muungano.

Mkataba huo umeibua mjadala wa kitaifa huku baadhi ya wanasiasa wakibeba ajenda na kuzunguka maeneo mbalimbali ya mikoa ya Tanzania Bara, wakipinga mkataba huo.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na ujumbe wa wawekezaji 11 kutoka Jamhuri ya Watu wa China, ukiongozwa na mkuu wa msafara huo, William Chu (kulia kwa Rais), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali kufanya mageuzi elimu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema serikali iko katika hatua ya mwisho kuanza utekelezaji wa mpango wake wa mageuzi makubwa katika sekta ya elimu.

Ni mpango unaohitaji ushiriki na jitihada za pamoja kutoka kwa wadau wa maendeleo katika kufanikisha vyema utekelezaji wake.

Othman aliyasema hayo ofisini kwake Migombani, mjini Zanzibar juzi alipokutana na kufanya mazungumza na Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulia Maendeleo ya Watoto (UNISEF), Elke Wisch.

Alisema Serikali ya Zanzibar inathamini jitihada za ushirikiano na shirika hilo katika kuendeleza sekta ya elimu hasa kwenye hatua za maandalizi ya watoto kupata elimu bora.

Othman alisema shirika hilo lina mchango mkubwa katika maeneo yanayohusu elimu, usafi wa mji na mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), jambo ambalo linaisaidia Zanzibar kupiga hatua kimaendeleo.

Aliliomba shirika hilo kuangalia uwezekano wa kusaidia masuala ya lishe kwa watoto wadogo shuleni ili kuepuka watoto kula vyakula vinavyotoka viwandani ambavyo huwekwa sukari nyingi, hivyo kuwaweka hatarini watoto.

Pia aliitaka jamii kubadili mfumo wa maisha ikiwamo kuepuka kuwazoesha watoto kula vyakula vyenye sukari nyingi ili kuepusha madhara ya kula vyakula vya namna hiyo.

Mwakilishi Mkaazi wa UNICEF Kanda ya Afrika Mashariki, Elke Wisch, aliahidi shirika litaendelea kuisaidia Zanzibar katika maeneo mbalimbali hasa kuandaa mazingira ya elimu bora kwa watoto ikiwa ni jitihada zake za kuunga mkono maendeleo ya Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIFAEL MESHACK LUKUMAY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CORONA** yenye usajili namba: **T 896 AQR,** CHASSIS NAMBA: **ST2100021033** na ENGINE NAMBA: **3S7793930.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/LON/499/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**LULU ALLY MANYILUZI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0277-0027** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SPRING VALLEY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0526-0525** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MRINGA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**POLISI TAARIFA: DAR/TAZ/RB/272413/2023**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO. 89/2019**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF**
**CHAMA CHA MAPINDUZI....................MDAI TUZO**

**DHIDI YA**
**MARTIN SENYE......................MDAIWA TUZO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: MARTIN SENYE**

Fahamu kwamba **THE REGISTERED TRUSTEES OF CHAMA CHA MAPINDUZI** amefungua shauri dhidi ya yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kusikiliza tarehe 06/09/2023 saa 2.30 asubuhi mbele ya T. Munzerere Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya Mjini.

Kumbuka: Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/ Muhuri wa baraza hili leo tarehe 21/08/2023

T. Munzerere
MWENYEKITI
21/08/2023

21/08/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN SELLA HAYGARU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOYA LANDCRUISER** yenye usajili namba **T 424 AKU,** CHASSIS NAMBA: **JTERB71J90009549** na ENGINE NAMBA: **1HZ20366407.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/ARU/577/2023**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.71 OF 2023**

**IN the Matter of the late SELESTINE SIMON SETEMBO**

**By 1. MAGDALENA SELESTINE SIMON**
**2..............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 28/08/2023.

Dated at Morogoro this 14th day of june 2023.

.................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**NYADHI INVESTMENT Co. LTD**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**M/MWANZO NYEHUNGE - SHAURI LA NDOA NA. 26/2022**

**PILI JOSEPH POLE _______________MDAI MUHUKUMIWA**
**DHIDI YA**
**SIMON GABRIEL KATWALE___________MDAIWA MUHUKUMI**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO NYEHUNGE, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA MOJA (1) ILIYOPO MTAKUJA MASHARIKI, SHAMBA EKARI MBILI NA NUSU LILILOPO NYAMADOKE - NYEHUNGE NA SHAMBA EKARI TATU LILILOPO BULALIGULU - NYEHUNGE. MNADA UTAFANYIKA MAHALI MALI ZILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA NA. 01 ILIYOPO MTAKUJA MASHARIKI | KATA YA NYEHUNGE - WILAYA YA SENGEREMA | 06/09/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | SHAMBA EKARI MBILI NA NUSU | NYAMADOKE - NYEHUNGE | 06/09/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | SHAMBA EKARI TATU | BULALIGULU - NYEHUNGE | 06/09/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. KWA MALI INAYOHAMISHIKA, MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI.
2. KWA MALI ISIYOHAMISHIKA, MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATES COURT OF TANZANIA**
**AT ARUSHA**
**TAXATION CAUSE NO.12.0F 2023**
**( C/F Civil Case No.18 of 2022**

**OLASITI INVESTMENT COMPANY LTD..D/HOLDER/APPLICANT**

**VERSUS**

**TO:**
**RASHID SEIF T/A IPTSAM TRANS.**

**NOTICE OF MENTION**

TAKE NOTICE that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrate Court of Arusha at Arusha on the 31st day of August,2023 at 7:50 AM in the morning.You may appear in person or your advocate.

TAKE FURTHER NOTICE that in default of your appearance on that day and time for mention,the Court may proceed in absence.

GIVEN under my HAND and seal the court this 16th of August,2023.

**Resident Magistrate**
**Arusha**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAUL THOMAS KADUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba **T 490** na ENGINE NAMBA: **2NZ3410861.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PJQ/DAR/UBU/3440/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......45/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: AMIRI ISSA HASSAN WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA kumteua msimamizi**
**YALIYOLETWA NA REHEMA BATONI PESA MBILI SIAME**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 24 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NEANEEMA JAMES KIMARO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba: **T 793 AND, CHASSIS NAMBA: LJ78009101 na ENGINE NAMBA: 2L2515188.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**KW/RB/3915/23**


# OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

# MOB: +255 - 0677020701

# E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

# WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI KITAIFA/KIMATAIFA

## Mwili wa mwasisi JKCI kuzikwa Ijumaa

**Na Christina Mwakangale**

MWILI wa aliyekuwa Mwasisi wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. William Mahalu, unatarajiwa kuzikwa Ijumaa mkoani Dar es Salaam.

Prof. Costa Mahalu, mdogo wa marehemu, alimwambia mwandishi wa habari hizi jana kuwa taratibu za maziko zinaendelea kufanyika. Msiba uko Mtaa wa Haile Selassie, Masaki, nyumba namba 100.

Prof. Mahalu ni miongoni mwa mabingwa watatu wa kwanza wa moyo nchini, waliosomeshwa na serikali nje ya nchi miaka ya 1970 kwa ajili ya kutoa tiba za kibingwa za moyo nchini.

Wengine ni Prof. Idrissa Mtulia na Pro. William Makene, aliyekuwa Daktari wa Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge katika taarifa yake juzi kwa vyombo vya habari, alisema Prof. Mahalu, ambaye ndiye mwasisi wa wazo la kuwa na taasisi hiyo, alifariki dunia usiku wa Agosti 20 mwaka huu, akiwa JKCI alikokuwa anapatiwa matibabu.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano JKCI, Anna Nkinda, alisema kwamba wanataaluma sekaya ya afya, wamejiandaa kwa ajili ya kuaga mwili wa bingwa huyo kesho, siku moja kabla ya maziko.

"Wanataaluma tunajiandaa kuaga Alhamisi saa saba. Tutakuwa na maandamano na utasomwa wasifu wake, kisha mwili utakabidhiwa kwa wanafamilia kwa ajili ya taratibu za kifamilia," alisema Anna.

Mei 21, 2008, Prof. Mahalu, alifanya upasuaji wa kwanza wa moyo nchini. Awali wagonjwa takribani 200 walitibiwa nje na kwa sasa ni asilimia tano pekee wanapelekwa nje kutokana na kuwapo JKCI.

Kwenye moja ya mahojiano na vyombo vya habari wakati wa uhai wake, Prof. Mahalu alisema: "Mwalimu Julius Nyerere alikuwa na nia ya nchi tuwe na hospitali yetu ya moyo, tukasomeshwa wataalamu nje, ila ikaonekana magonjwa ya moyo si kipaumbele.

"Ili nisipoteze taaluma yangu, nikaenda Zimbabwe wakati Rais ni Robert Mugabe, ikaanzishwa taasisi ya moyo, ila alikuja Rais Mwinyi (Ali Hassan) Zimbabwe akaambiwa 'kuna kijana wako anafanya vizuri', nikaitwa... baadaye nikarudi nchini."

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo na Upasuaji kutoka JKCI, Dk. Evarist Nyawawa, alisema amemfahamu Prof. Mahalu kama mmoja wa mabingwa wa moyo wa kwanza nchini.

"Prof.Mahalu ni mzalendo. Baada ya kurejea nchini alitoka Uingereza kusoma, aliamua kutibua Watanzania, lakini kutokana na vipaumbele vya nchi wakati huo kutoweka magonjwa ya moyo kwenye kipaumbele, alikwenda Zimbabwe kufanya kazi.

# Trump: Nitajisalimisha Alhamisi



Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump (katikati). **PICHA: MTANDAO**

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, amesema atajisalimisha kwenye mamlaka katika jimbo la Georgia kesho ili kujibu mashtaka katika kesi inayomtuhumu kwa kupanga njama kinyume cha sheria ya kugeuza matokeo ya uchaguzi wa urais wa mwaka 2020 katika jimbo hilo.

Trump aliyabainisha hayo jana kupitia mtandao wake wa kijamii, saa chache baada ya jaji mmoja wa Georgia, Juma matatu kuidhinisha dhamana ya dola 200,000 katika kesi ya ulaghai iliyowasilishwa dhidi yake katika jimbo hilo.

Trump na wengine 18 katika kesi hiyo wamepewa muda wa hadi Ijumaa saa sita mchana wawe wamejisalimisha katika mamlaka huko Georgia ili kusomewa mashtaka.

"Unaweza kuamini? Nitaenda Atlanta, Georgia, siku ya Alhamisi kukamatwa," alisema Trump.

Itakuwa ni mara ya nne kwa Trump kukamatwa tangu Aprili, alipokuwa rais wa kwanza wa zamani katika historia ya Marekani kukabiliwa na mashtaka.

Mbali na suala hilo, Jaji wa Mahakama ya Kaunti ya Fulton Scott McAfee aliweka masharti kadhaa katika makubaliano yaliyoidhinishwa na waendesha mashtaka na mawakili wa Trump.

"Mshtakiwa hatafanya kitendo chochote cha kumtisha mtu yeyote anayejulikana kwake kuwa mlalamishi au shahidi katika kesi hii au kuzuia utoaji wa haki kwa njia yoyote," alisema McAfee.

Alisema vitisho kama hivyo vitajumuisha kuchapisha jumbe za mitandao ya kijamii, au kutuma vitisho kama hivyo vikiwa vimechapishwa na mtu mwingine.

McAfee aliweka dhamana ya dola 100,000 kwa kila mmoja kwa washitakiwa wengine wawili katika kesi hiyo wakiwemo mawakili wa zamani wa kampeni ya Trump, John Eastman na Kenneth Chesebro. **VOA**

# Ma-RC waonya uvujishaji siri za serikali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kuzingatia maadili, nidhamu na utunzaji wa siri za serikali kipindi hiki cha utandawazi.

Pia amewataka kuongoza maeneo yao kwa njia shirikishi bila kuingiliana katika utendaji wao na kuikumbuka sekta binafsi pale wanapohitaji kuwezeshwa katika shughuli mbalimbali za mkoa.

Dk. Mpango alielekeza hayo jana katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Kibaha Kwamfipa, mkoaji Pwani wakati akifungua mafunzo ya uongozi kwa wakuu wa mikoa na makatibu tawala Tanzania Bara.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kuongeza jitihada ya kuwezesha sekta binafsi na pia, kuhakikisha wanasoma na kuzielewa nyaraka muhimu za serikali.

Alisema dhima ya mafunzo hayo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ambayo inaeleza umuhimu wa kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa hali shirikishi.

"Nimefurahi maudhui ya mada zote zitakazowasilishwa yanalenga kuboresha utendaji kazi kwa wakuu wa mikoa na makatibu tawala na mada zote zitakazotolewa ni nzuri na zitakazoboresha utendaji wenu.

"Upo upungufu na malalamiko kutoka mikoa mnayoongoza. Ipo mifano ambayo ni kutokuzingatia mipaka ya utendaji kazi ambayo inatokana na baadhi ya wakuu wa mikoa kutaka kuwa maofisa masurufu," alisema.

Dk. Mpango alitoa mfano mingine ni kasi ndogo ya utatuzi wa migogoro na kushughulikia baadhi ya kero za wananchi, kutosikiliza sekta binafsi huku akiwaeleza kuwa jitihada mahususi zinahitajika kuvutia wawekezaji.

Aliwataka kushughulikia kero za wananchi, wakiwamo wanaoandika barua kwao, wakitaka kutatuliwa kero zao kwa wakati na kuwasisitiza suala la utunzaji siri za serikali, hasa kipindi hiki cha utandawazi, pia utunzaji wa mazingira.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa yote Tanzania Bara ili wawe na uwezo wa kusimamia wananchi.

Alitaja malengo mengine ni kuwawezesha kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku na kuboresha utendaji kazi wao.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema kundi hilo ni kiungo muhimu katika utendaji wao na linawakilisha utekelezaji wa sera.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema kuwa baada ya mafunzo hayo, anatarajia kuanza utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa sambamba na kuimarisha uongozi na kutunza siri za serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, aliyataja ni mafunzo ya kudhibiti masuala ya kibinadamu na taratibu za sheria na kanuni katika uongozi.

Alisema katika mkoa wake, hawaingiliani katika majukumu yao na kuahidi kufanyia kazi wanayofundishwa katika mafunzo hayo.

# MOROCCO AANIKA MBINU KUISHIKA MASHUJAA FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold FC, Hemed Suleiman 'Morocco', amesema suluhu waliyoipata kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma dhidi ya timu machachari ya Mashujaa FC ni kutokana na kuwazuia kucheza staili yao ya kupiga mipira mirefu ya juu kwani nguvu yao ndipo ilipo.

Akizungumza juzi mara baada ya kumalizika mechi hiyo ya raundi ya pili ya Ligi Kuu, Morocco alisema kilichoisaidia timu yake kuondoka salama Kigoma ni kuwazuia Mashujaa kucheza soka lao walilozoea la kutumia nguvu nyingi na kupiga mipira mirefu.

"Nashukuru Mungu pamoja na kuwapongeza wachezaji wangu kwa sababu wamecheza kwa bidii sana, wamecheza soka la kasi ambalo nilitegemea kuwa litaonesha leo (juzi) kwenye uwanja huu, kwa sababu wapinzani wetu niliwasoma wanacheza soka la nguvu pamoja na kupiga mipira mirefu ya juu, hivyo niliwatengeneza vijana wangu wawe wanakimbia sana, kuziba mianya na kuzuia mipira yote mirefu isiwafikie walengwa," alisema Morocco.

**Pamoja na hayo, Morocco alisema wao walijaribu kuweka mpira chini na kadri muda ulivyozidi kwenda mbele ndivyo wachezaji wake walivyozidi kuumiliki mpira, jambo ambalo linamfanya kuona mwanga mzuri kwenye kikosi chake kuelekea mechi zijazo.**

Mohamed Abdallah 'Bares', Kocha Mkuu wa Mashujaa, yeye alisema safu yake ya ushambuliaji kwa mechi ya juzi haikuwa makini kwani walitengeneza nafasi ambazo hazikutumiwa vema.

"Huu ndiyo mpira, tumepata suluhu, hatukutumia nafasi tulizozipata, safu ya ushambuliaji haikuwa makini, lakini tutakwenda kulifanyia kazi mazoezini," alisema.

Suluhu hiyo inazifanya timu hizo kufikisha pointi nne kila moja, huku ikiwa ni sare ya kwanza kwa Mashujaa ikiwa uwanja wake wa nyumbani baada ya kushinda mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar mechi ya awali, Geita Gold yenyewe iliidungua Ihefu FC bao 1-0 ugenini.

**NAKUTOKA...**



Mshambuliaji wa timu ya soka ya Wafanyakazi wa Hospitali ya Muhimbili, Abdallah Mtagwa (kulia), akitafuta njia ya kumtoka beki wa timu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Lameck Lima, katika mchezo wa fainali ya mashindano ya 'Samia Afya Cup 2023' uliochezwa katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. TRA ilitwaa ubingwa huo baada ya kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-2 kutokana na dakika 90 za mchezo kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: Anjella Mndolwa (TURDACO)**

# JKT Tanzania yakimbilia Shinyanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya JKT Tanzania imetangaza rasmi kuwa itautumia Uwanja wa Kambarage Shinyanga kama dimba lake la nyumbani katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara, pindi utakapofunguliwa na Bodi ya Ligi nchini, TPLB.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Kapteni Speratus Ngemeke Lubinga, amesema jana kuwa wameamua hivyo baada ya kupokea ombi kutoka serikali ya mkoa huo pamoja na mashabiki wa soka mkoani Shinyanga.

Timu hiyo iliyopanda daraja msimu huu kutoka Championship, ilikuwa inautumia Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo uliopo Mbweni, Dar es Salaam, kwenye mechi zake mpaka ilipofanikiwa kupanda Ligi Kuu.

"Tuliitikia wito kutoka Serikali ya Mkoa wa Shinyanga, lakini pia tuliitikia wito wa Bodi ya Ligi, baada ya kupita kuukagua uwanja walituambia tuwe karibu na wamiliki wa uwanja ambao kwa sasa wanautengeneza kwa ajili ya matumizi ya Ligi Kuu, na baada ya maelekezo hayo tuliwasiliana na mkoa, wakatuambia twende tukaone hayo marekebisho ambayo Bodi ya Ligi wanataka yafanyike," alisema katibu huyo.

Alisema iwapo utafunguliwa, watacheza mechi zao zote za nyumbani msimu huu mkoani humo.

Timu hiyo tayari imecheza mechi moja tu ikiwa ugenini Jumanne iliyopita, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi dhidi ya Namungo FC na kupata ushindi wa bao 1-0.

Mmoja wa wanaosimamia uwanja huo ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema TPLB iliwashauri kuondoa vipara viwili uwanjani hapo ambavyo vilikuwa maeneo ya kupigia kona na tayari wameshapanda nyasi, sehemu ya benchi ya kukaa makocha na wachezaji wa akiba na kwenye vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji.

Habari kutoka Shinyanga zinasema tayari wakaguzi wameshafanya kazi yao na kujiridhisha, hivyo wakati wowote unaweza kuruhusiwa kutumika kwenye mechi za Ligi Kuu.

# Wacheza gofu 100 wathibitisha CDF Trophy Open 2023

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI 100 wa gofu wamethibitisha kushiriki mashindano ya wazi ya mchezo huo, CDF Trophy Open 2023, yatakayofanyika Septemba 2-3, mwaka huu katika viwanja vya Klabu ya Gofu Lugalo, Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Brigedia mstaafu Michael Luwongo, alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu zote nchini.

Alisema mashindano hayo yana lengo la kuazimisha siku ya kuzaliwa kwa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ ), ambalo lilianzishwa Septemba Mosi, 1964 pamoja na kumuenzi Mkuu wa Majeshi Tanzania, Jacob Mkunda.

"Tukiwa tunaadhimisha siku hiyo tumeandaa mashindano ambayo yatashirikisha klabu zote za gofu hapa nchini, mpaka sasa wachezaji 100 wamethibitisha kushiriki.

"Pia tunawashukuru na kuwapongeza wadhamini wetu kwa ushiriki wao katika mashindano haya, ambayo yatakuwa ya wazi yakishirikisha timu za Jeshi la Tanzania, Malawi na timu za kiraia, yakitanguliwa na Combat Fiddle Ijumaa ya Septemba Mosi.

"Malawi ambao walishiriki pia mwaka jana, watakuja na timu za Jeshi lao, lakini pia Klabu ya Gofu ya Lilongwe (Lilongwe Golf Club) ambayo ni ya kiraia, msafara wao utajumuisha takribani washiriki 20, huku tayari washiriki wa ndani wapatao 100 wakiwa wameshajisajili," alisema Luwongo na kuongeza:

"CDF Trophy ni shindano la kipekee kabisa, ambalo litakuwa na zawadi nzuri zilizoboreshwa zaidi kwa ajili ya washindi wa kategori zote za 'Professional,' Watoto (Juniors), Divisheni za A, B na C, pamoja na wanawake na 'seniors.'

"Tutaitumia CDF Trophy kuiandaa Timu ya Taifa ya Tanzania ya Gofu itakayoshiriki Mashindano ya Jumuiya ya Madola, huko San Diego, Marekani, ambako Tanzania itakuwa nchi pekee kuiwakilisha Afrika."

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Gilman Kasiga, alisema wataendelea kushirikiana na wadhamini wao wote wakiwa na lengo la kuuendeleza mchezo huo.

**CDF Trophy ni shindano la kipekee kabisa, ambalo litakuwa na zawadi nzuri zilizoboreshwa zaidi kwa ajili ya washindi wa kategori zote.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich na Liverpool zinamwania kiungo wa England, Kalvin Phillips mwenye wa miaka 27, kutoka Manchester City. ***(90min)***

### DOKU ANUKIA CITY

MANCHESTER City imefikia makubaliano ya maslahi binafsi na Jeremy Doku juu ya mkataba wa muda mrefu ambapo ada yake imetajwa kuwa euro milioni 60 iliyokubaliwa na Rennes kwa winga huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 21. ***(Fabrizio Romano)***

### PAQUETA BASI TENA

KLABU ya West Ham ilifikia makubaliano ya pauni milioni 85 na Manchester City kwa ajili ya kumuuza Lucas Paqueta kabla ya uhamisho huo kusambaratika kutokana na kiungo huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 25 kuchunguzwa kwa ukiukaji wa kanuni za kamari. ***(Mail)***

### BALEBA ANUKIWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inakaribia kukamilisha usajili wa pauni milioni 25 wa kiungo wa kati wa Lille raia wa Cameroon, Carlos Baleba mwenye umri wa miaka 19. ***(Talksport)***

### SOLANKE NA WEST HAM

KLABU ya West Ham imewasilisha ombi rasmi la takribani pauni milioni 35 kumnunua mshambuliaji wa Bournemouth, Dominic Solanke, 25. ***(Football Insider)***

### MBAPPE KUSHAWISHIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain bado ina matumaini inaweza kumshawishi Kylian Mbappe kuongeza mkataba wake baada ya mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24 kukutana na maofisa wa kundi la umiliki wa klabu hiyo ya Qatar, licha ya mchezaji huyo kuhusishwa na kuhamia Real Madrid mkataba wake utakapokamilika msimu wa majira ya joto. ***(Diario AS)***

### EN-NESYRI AWINDWA

KLABU ya West Ham inafanya mazungumzo na Sevilla kuhusu usajili wa mshambuliaji wao wa Morocco, Youssef En-Nesyri mwenye umri wa miaka 26. ***(90min)***

### PETROVIC SAFI CHELSEA

CHELSEA imekubali mkataba wa pauni milioni 14 kwa mlinda mlango wa New England Revolution raia wa Serbia, Djordje Petrovic, 23. ***(Mail)***

### ODOI LULU FULHAM

KLABU ya Fulham inakabiliwa na changamoto mpya kumpata Callum Hudson-Odoi wa Chelsea baada ya Everton na Nottingham Forest kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili winga huyo wa zamani wa England mwenye umri wa miaka 22. ***(Standard)***

### BALOGUN ANUKIA CHELSEA

CHELSEA bado ipo kwenye mazungumzo kuhusu uhamisho wa Folarin Balogun wa Arsenal, licha ya mshambuliaji huyo wa Marekani mwenye umri wa miaka 22, kufikia makubaliano ya maslahi binafsi na 'The Blues' hao. ***(Football Transfers)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AKERWA MATUMIZI SHERIA YA KUPOTEZA MUDA

**LONDON,** England

MIKEL Arteta huenda 'alipenda' ushindi mwembamba wa Arsenal dhidi ya Crystal Palace Jumatatu, lakini anaamini kuzingatia muda kunaweza kuhitajika ili kuondoa kutofautiana kwa upotevu wa muda baada ya Takehiro Tomiyasu kukiuka sheria.

**'Washikabunduki' hao walishinda 1-0 kwa bao la mkwaju wa penalti la Martin Odegaard katika kipindi cha pili.**

Beki wa Japan, Tomiyasu alitolewa nje kwa kadi nyekundu katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Selhurst Park, baada ya kupata kadi ya pili ya njano kwa kumchezea vibaya Jordan Ayew dakika saba tu baada ya kuonywa kwa kudhaniwa kuwa anapoteza muda.

Sheria mpya ya msimu huu na miongoni mwa mabadiliko mengine, ni kuzuia upotevu wa muda, lakini Arteta anaamini kuwa muda huo haukujumuisha nafasi ya Tomiyasu.

Alipoulizwa kuhusu mabadiliko ya sheria, Mhispania huyo alijibu: "Kwangu mimi sio suala. Mwamuzi aliamua kupiga filimbi.

"Na sisi ni sambamba na hilo. Kitu pekee tunachoomba ni uthabiti. Ikiwa sivyo, tunahitaji kucheza na saa ili kuelewa ni nini kinachotakiwa na kisichotakiwa.

**●●● Kitu pekee tunachoomba ni uthabiti, ikiwa sivyo, tunahitaji kucheza na saa ili kuelewa...**

Arteta hakukubali alipoambiwa Tomiyasu alisubiri kwa sekunde 23 kabla ya kuonywa - akijibu: 'Haikuwa hivyo. Nadhani ilikuwa sekunde nane. Huenda tukalazimika kucheza na saa ya kusimamishwa. Hivi ndivyo viwango.'

Licha ya kadi nyekundu, Arsenal walishinda kwa mara ya pili mfululizo msimu huu baada ya ushindi dhidi ya Nottingham Forest kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,146,3

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
KMC
1 | 1.21
X | 5.56
2 | 11.91

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GREENWOOD ATEMWA RASMI MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imethibitisha kuwa imefikia makubaliano na Mason Greenwood kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ataendelea na soka lake nje ya klabu hiyo.

Greenwood alisimamishwa na United Januari 2022 baada ya kushtakiwa kwa ubakaji na unyanyasaji, lakini mashtaka yote dhidi yake yalitupiliwa mbali Februari, mwaka huu.

Baada ya polisi kuhitimisha kesi yao dhidi ya Greenwood, United ilifungua uchunguzi wao wa ndani na kumchunguza mshambuliaji huyo, ikiwa ni pamoja na mkataba wa mkopo na Atalanta ambao haukufanikiwa.

United sasa wamemaliza uchunguzi wao na wamefikia makubaliano na Greenwood kuachana.

"Manchester United imehitimisha uchunguzi wake wa ndani kuhusu tuhuma zilizotolewa dhidi ya Mason Greenwood," taarifa ya klabu ilisema.

"Mchakato wetu ulianza Februari 2023, kutokana na mashtaka yote dhidi ya Mason kufutwa. Kwa muda wote, tumezingatia matakwa, haki na mtazamo wa mtuhumiwa pamoja na viwango na maadili ya klabu, na tulitaka kukusanya taarifa ya kina. Hii imetutaka kuendelea kwa usikivu na uangalifu ili kupata ushahidi usio na shaka, ikiwa ni pamoja na kutoka kwa wale wenye ujuzi wa moja kwa moja wa kesi hiyo.

"Kulingana na ushahidi uliopatikana kwetu, tumehitimisha kuwa nyenzo zilizochapishwa mtandaoni hazikutoa picha kamili na kwamba Mason hakufanya makosa ambayo alishtakiwa hapo awali.



# Pulisic aanza maisha Serie A

**MILAN,** Italia

NYOTA wa Marekani, Christian Pulisic, alianza maisha yake kule AC Milan kwa mtindo wa kuvutia kwa kufunga bao moja na kutengeneza jingine huku Bologna ikichapwa mabao 2-0 Jumatatu kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Serie A.

Pulisic, ambaye alijiunga na Milan mwezi uliopita, alichangia bao la kwanza la Olivier Giroud na mchezaji mwenzake wa zamani wa Chelsea na yeye akatengewa pasi na kufunga bao dakika ya 21.

"Ulikuwa mwanzo mzuri kwa hakika," alisema Pulisic.

"Nimefurahi sana kuwa sehemu ya timu hii. Mabao mawili ya mapema yalitusaidia sana kwa sababu ulikuwa mchezo mgumu baada ya hapo. Na kwangu ni mwanzo mzuri na binafsi pia, mzuri kupata bao."

Pulisic ni mojawapo ya sura mpya pale 'Rossoneri' ambapo klabu ... ilikuwa yenye shughul... ingi zaidi Serie A, ikis... wachezaji sita wapya.

Pulisic alisema uw... wa wachezaji wenzake ... zamani ulichangia ka... uamuzi wake wa kujiu... na klabu hiyo maaruf... Italia.

"Ilikuwa tu kuzungu... na watu hao," Pulisic a... ma. "Na Olivier tulik... na uzoefu mzuri pam... nilicheza na Fikayo ... mori), nilicheza na Ru... (Loftus Cheek).

22,426/-

# KMKM FC YAPANIA KUPINDUA MEZA KWA ST GEORGE ETHIOPIA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kupoteza mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika tena wakiwa nyumbani, wawakilishi wa Zanzibar kwenye michuano hiyo, KMKM wamesema wanamatumaini makubwa ya kwenda kupindua matokeo ugenini na kutinga raundi ya kwanza.

Katika mchezo wa awali uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ambao KMKM inautumia kama uwanja wake wa nyumbani kutokana na ule wa Amaan visiwani Zanzibar kuwa katika matengenezo, ilikubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya St George ya Ethiopia.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ame Msimu, alisema tayari wamefanyia kazi mapungufu yote waliyoyaona katika timu yao kwenye mchezo wao uliopita, hivyo ana matumaini ya kufanya vizuri ugenini.

**Alisema mapungufu makubwa waliyoyaona katika mchezo huo ni wachezaji kutozitumia vizuri nafasi walizotengeneza pamoja na kukosa umakini hasa wanapokuwa katika lango la mpinzani wao.**

Alisema tayari mapungufu hayo yamefanyiwa kazi ikiwamo kuwapa somo la saikolojia wachezaji kutokuwa na hofu ya mchezo hasa wakiwa ugenini ili kutimiza lengo lao.

Hata hivyo, alisema timu hiyo itaendelea na kambi yake Tanzania Bara hadi watakapoelekea Ethiopia katika mchezo wa marudiano.

KMKM itashuka dimbani ugenini nchini Ethiopia Jumamosi wiki hii, ikihitaji kupata ushindi kuanzia mabao 2-0 ili kuweza kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu.



Vijana wakicheza mpira katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gamondi kupeleka moto

INATOKA UKURASA 24

kutafuta matokeo chanya.

"Benchi la ufundi limemaliza kazi yake, jukumu lililobaki ni kwetu wachezaji kuanza msimu vizuri kwa kusaka pointi tatu muhimu dhidi ya KMC FC, tunatambua ubora wa wapinzani wetu, lakini kikubwa tupo kwa ajili ya kuonesha ushindani na kufikia malengo yetu ya kuanza vizuri ligi," alisema Nkane.

Kocha Mkuu wa KMC FC, Moallin alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kukabiliana na Yanga ili kupata matokeo mazuri.

Alisema wametoka katika mechi ngumu dhidi ya Namungo FC na leo wanaenda kucheza mchezo mgumu mwingine dhidi ya Yanga ambao ni mabingwa wa msimu uliopita.

"Yanga ni timu kubwa iko vizuri kiuchezaji tunaenda kukutana na timu ngumu na ninatarajia kucheza mchezo wa kimbinu na kiufundi zaidi dhidi ya wapinzani wetu hao," alisema Moallin.

Nahodha wa KMC FC, Awesu Awesu, alisema wanakutana na timu kubwa lakini hawaogopi bali watacheza kwa kuwaheshimu na wamechukua tahadhari zote dhidi ya Yanga.

## Simba, Yanga

INATOKA UKURASA 24

wa nazo usajili wa mwisho ulikuwa kipa Ayoub Lakred, lakini kwa sasa siwezi kumaliza maneno.

"Lakini kama watu wanasema wameonekana viongozi wangu wapo na Msuva wanafanya mazungumzo, basi watakuwa wanataka kufanya maamuzi yatakayokuwa sahihi, hakuna timu ambayo haitaki kuwa na winga huyo anayeweza kucheza pia kama mshambuliaji.

"Ni mchezaji mzuri kijana wa nyumbani, mwenye uwezo mkubwa na analifahamu soka la Tanzania, ukiwa naye ina maana umejihakikisha kuwa na mchezaji bora, ila tusubiri taarifa kutoka kwa uongozi wa juu," alisema Ahmed.

Alipotafutwa Msuva alisema kwa sasa hawezi kuzungumzia suala lolote kuhusiana na taarifa hizo za kuhusishwa na klabu hizo kuhitaji huduma yake.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/08/23 | 17:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.26 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/08/23 | 18:30 | Cadiz CF vs UD Almeria | 2.23 | 3.25 | 3.05 |
| 03. 26/08/23 | 20:00 | SC Farense vs GD Chaves | 2.36 | 3.10 | 3.00 |
| 04. 26/08/23 | 20:30 | Granada CF vs RCD Mallorca | 2.55 | 2.90 | 2.95 |
| 05. 26/08/23 | 21:45 | KV Kortrijk vs Standard Liege | 2.95 | 3.45 | 2.21 |
| 06. 26/08/23 | 22:00 | Excelsior Rotterdam vs Fortuna Sittard | 2.22 | 3.50 | 2.90 |
| 07. 27/08/23 | 02:30 | New York Red Bulls vs Inter Miami CF | 2.40 | 3.30 | 2.50 |
| 08. 27/08/23 | 13:15 | PEC Zwolle vs FC Utrecht | 2.90 | 3.60 | 2.21 |
| 09. 27/08/23 | 16:00 | Strasbourg Alsace vs Toulouse FC | 2.09 | 3.50 | 3.20 |
| 10. 27/08/23 | 16:30 | FSV Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.48 | 3.45 | 2.55 |
| 11. 27/08/23 | 17:00 | St. Truidense VV vs Cercle Brugge | 3.05 | 3.30 | 2.23 |
| 12. 27/08/23 | 17:00 | St Mirren FC vs Aberdeen FC | 2.41 | 3.20 | 2.85 |
| 13. 27/08/23 | 17:30 | Boavista Porto vs Casa Pia Lisbon | 2.22 | 3.15 | 3.20 |
| 14. 27/08/23 | 17:45 | SC Heerenveen vs Sparta Rotterdam | 2.26 | 3.50 | 2.85 |
| 15. 27/08/23 | 18:00 | Racing Club de Ferrol vs Sporting Gijon | 2.31 | 3.00 | 3.20 |
| 16. 27/08/23 | 18:00 | Sandefjord Fotball vs FK Haugesund | 2.21 | 3.20 | 2.80 |
| 17. 27/08/23 | 18:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.11 | 3.75 | 2.95 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 23/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2590 | Gareji vs FC Spaeri | 1.42 | 4.38 | 5.90 |
| 16:00 | 5617 | FC Norchi Dinamo Tbilisi vs Sioni Bolnisi | 3.10 | 3.56 | 2.01 |
| 18:00 | 1934 | MKS Swit Nowy Dwor Mazowiecki vs Jagiellonia II Biaystok | 1.80 | 3.67 | 3.67 |
| 18:00 | 2463 | Concordia Elblag vs Olimpia Zambrow | 1.98 | 3.46 | 3.26 |
| 18:00 | 3042 | Usti N Orlici vs FK Viktoria Zizkov | 5.90 | 4.58 | 1.40 |
| 18:00 | 4066 | Unia Skierniewice vs GKS Wikielec | 1.71 | 3.77 | 3.98 |
| 18:00 | 4156 | Kszo Ssa Ostrowiec Sw. vs MKS Podlasie Biala Podlaska | 2.46 | 3.25 | 2.59 |
| 18:00 | 4295 | Richards Bay FC vs Mamelodi Sundowns | 5.86 | 3.66 | 1.55 |
| 18:00 | 4399 | Ararat Armenia vs Pyunik Yerevan | 2.50 | 2.99 | 2.73 |
| 18:00 | 4657 | Tj Slovan Vistuk vs FC Rohoznik | 3.06 | 4.28 | 1.85 |
| 18:00 | 4788 | Loko Kosice vs Slavia TU Kosice | 3.11 | 4.49 | 1.80 |
| 18:00 | 4812 | KS Gornik Polkowice vs Starowice | 1.49 | 4.58 | 4.79 |
| 18:00 | 4872 | FK 09 Bacuch vs TJ Medzibrod | 5.12 | 5.53 | 1.38 |
| 18:00 | 4943 | SK Nova Dedinka vs FK Slovan Galanta | 9.61 | 5.32 | 1.24 |
| 18:00 | 5524 | TJ Visnove vs OFK Rosina | 2.75 | 3.87 | 2.09 |
| 18:00 | 5635 | FK Iskra Hnusta vs SK Odeva Lipany | 16.34 | 9.40 | 1.07 |
| 18:00 | 5644 | Aquacity Poprad vs FK Humenne | 4.77 | 4.36 | 1.51 |
| 18:30 | 1721 | Lechia Tomaszow Mazowiecki vs KS Pelikan Lowicz | 1.97 | 3.51 | 3.26 |
| 18:30 | 2016 | Pilica Bialobrzegi vs Legionovia | 3.52 | 3.82 | 1.80 |
| 18:30 | 3143 | Sokol Kleczew vs KP Starogard Gdansk | 2.08 | 3.56 | 2.95 |
| 19:00 | 1257 | Ilves Tampere vs AC Oulu | 2.11 | 3.25 | 3.14 |
| 19:00 | 1583 | Mjondalen vs Jerv | 2.40 | 3.28 | 2.58 |
| 19:00 | 2316 | Raufoss vs Sogndal | 2.36 | 3.37 | 2.57 |
| 19:00 | 2321 | IK Start vs Aasane Fotball | 1.62 | 3.89 | 4.25 |
| 19:00 | 3467 | Kolkheti Poti-Dinamo vs 2 Tbilisi | 1.71 | 4.16 | 3.66 |
| 19:00 | 4099 | Kongsvinger IL vs Fredrikstad | 2.24 | 3.23 | 2.83 |
| 19:00 | 4282 | PPJ vs Lahden Reipas | 2.23 | 3.66 | 2.64 |
| 19:00 | 4455 | Kfum Oslo vs Hodd | 1.45 | 4.04 | 5.86 |
| 19:00 | 4944 | Loko Tbilisi vs FC Kolkheti Khobi | 3.05 | 3.35 | 2.04 |
| 19:00 | 4971 | Young Africans vs KMC | 1.21 | 5.56 | 11.91 |
| 19:00 | 5303 | Kristiansund vs Sandnes Ulf | 1.60 | 3.93 | 4.33 |
| 19:00 | 5425 | Bryne vs Moss | 2.07 | 3.38 | 3.03 |
| 19:30 | 5196 | Spartak Trnava vs SC Dnipro 1 | 2.14 | 3.39 | 3.14 |
| 19:45 | 2603 | Hibernian vs Aston Villa | 9.03 | 5.42 | 1.27 |
| 20:00 | 1790 | Bron Radom vs Legia II Warszawa | 3.96 | 3.81 | 1.71 |
| 20:00 | 3146 | Jahn Regensburg vs Borussia Dortmund II | 1.85 | 3.57 | 3.83 |
| 20:00 | 3631 | Viktoria Koln vs RW Essen | 2.16 | 3.46 | 3.05 |
| 20:00 | 4574 | Sonderjyske vs HB Koge | 1.30 | 4.85 | 7.28 |
| 20:00 | 5052 | Saarbrucken vs Verl | 1.65 | 3.88 | 4.66 |
| 20:00 | 5242 | FC Helsingor vs Hillerod | 1.69 | 3.73 | 3.98 |
| 20:00 | 5530 | Erzgebirge Aue vs Sandhausen | 2.81 | 3.38 | 2.33 |
| 20:00 | 5547 | Vendsyssel FF vs Kolding IF | 2.26 | 3.39 | 2.68 |
| 20:00 | 5921 | Freiburg II vs Unterhaching | 1.69 | 3.73 | 4.56 |
| 20:30 | 2398 | Cape Town City vs Sekhukhune United | 2.02 | 2.93 | 3.96 |
| 22:00 | 1562 | Sporting Braga vs Panathinaikos | 1.72 | 3.34 | 4.77 |
| 22:00 | 2693 | Maccabi Haifa vs BSC Young Boys | 2.30 | 3.41 | 2.76 |
| 22:00 | 2890 | Molde vs Galatasaray | 2.75 | 3.40 | 2.39 |
| 22:00 | 5589 | Pfa Antioquia FC vs AD Carmelita | 2.95 | 3.35 | 2.16 |
| 23:00 | 1238 | Vargas Torres vs Imbabura Sporting Club | 2.70 | 2.96 | 2.55 |
| 23:00 | 3450 | 9 De Octubre FC vs America | 2.06 | 3.11 | 3.42 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Agosti 23, 2023

Nipashe




Greenwood atemwa Man Utd

UKURASA 22

# Simba SC, Yanga vita vikali saini ya Msuva

●●● Milioni 750 zatakiwa mezani, mwenyewe asema atakuwa...

**Na Saada Akida na Adam Fungamwango**

MIAMBA ya soka nchini, Simba na Yanga, imeingia katika mbio mpya za usajili baada ya kila moja kutaka kuinasa saini ya winga fundi Mtanzania Simon Msuva, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru, imeelezwa.

**Msuva anayeichezea timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kwa sasa hana timu yoyote baada ya kumaliza mkataba wa mwaka mmoja na timu ya Al-Qadsiah ya Saudi Arabia.**

Mbali na timu hiyo, mchezaji huyo amewahi kuzichezea Klabu za Wydad Athletic Club ya Casablanca nchini Morocco, Difaa El Jadida pia ya huko, Yanga, Moro United, baada ya kuanzia soka lake kwenye kikosi cha pili cha Azam FC.

Dirisha la usajili wa ndani lipo wazi hadi Agosti 31, mwaka huu, lakini Simba bado inaruhusiwa kusajili mchezaji yeyote kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kwani Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), lilitoa ruhusa kwa klabu zote ambazo hazichezi raundi ya awali kuendelea kusajili.

Hata hivyo, kama Yanga ikifanikiwa kuinasa saini ya Msuva, ataendelea tu kuichezea kwenye Ligi Kuu huku michuano ya CAF, kama timu hiyo itatinga hatua ya makundi ndipo dirisha la usajili kwa klabu zilizoanzia raundi ya awali litakuwa wazi tena.

Simba na Yanga zimekuwa zikipambana kunasa saini ya Msuva, lakini kikwazo kikubwa kinaelezwa ni dau la Sh. milioni 750 anazotaka ili kumwaga wino.

Yanga wanahaha kumpata mtu sahihi katika eneo la mwisho la ushambuliaji baada ya washambuliaji waliopo, Kennedy Musonda, Clement Mzize na Hafiz Konkoni, kushindwa kuonyesha makali yao.

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya Yanga zinaeleza kuwa mpaka sasa, Msuva amewaambia Yanga anataka dau la Sh. milioni 750 ikiwa wanataka kumuona akisaini kuichezea timu yao dau ambalo limekuwa kubwa kwao licha ya kuwapo kwa mazungumzo mengine na Simba ambao bado wanapambana kuhakikisha wanapata saini yake.

Nipashe lilipomtafuta Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema hawezi kusema lolote kuhusu usajili wa winga huyo kwa sababu dirisha la usajili lipo wazi na kwamba ni mchezaji mzuri na kila timu ingehitaji kupata huduma yake.

"Msuva sina uhakika sana kwa sababu ninaona taarifa kwenye mtandao, ni mchezaji mzuri na ukiwa naye anaweza kusaidia lakini tusubiri uongozi wa juu, kwa taarifa nilizoku-

INAENDELEA UKURASA 23




MSUVA

## Gamondi kupeleka moto wa CAF KMC

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya ASAS ya Djibouti, timu ya Yanga imesema moto huo sasa wanakwenda kuuendeleza leo katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC, utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Yanga ambao watakuwa wenyeji wa mchezo huo, watawakaribisha wapinzani wao, KMC, ambao mcheo wao wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu walilazimisha sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Namungo FC.

Kikosi cha Yanga kinashuka dimbani kikihitaji kuanza vizuri katika mchezo huo ili kuendeleza rekodi ya msimu uliopita ya kuanza msimu kwa ushindi, lakini pia kikipania kutetea taji lao hilo.

Timu zote zimeanza msimu zikiwa na benchi jipya la ufundi wakati Yanga ikinolewa na Kocha raia wa Argentina, Miguel Angel Gamondi, KMC FC ipo chini ya Msomalia mwenye uraia wa Marekani, Abdihamid Moallin, aliyewahi kukinoa kikosi cha Azam FC.

Kuelekea mchezo huo wa leo Kocha wa Yanga, Gamondi alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo ya kwanza kwao ya Ligi Kuu msimu.

Alisema baada ya kumalizika kwa mechi ngumu ya kimataifa wikiendi iliyopita, leo wanashuka dimbani katika mchezo mwingine wa ushindani mkubwa wakihitaji pointi tatu muhimu.

"Nimefanikiwa kuona baadhi ya mechi za KMC FC, tumefanya maandalizi mazuri tumefanyia kazi na tuko tayari kwa mchezo huo kusaka pointi tatu muhimu," alisema Gamondi.

Aliwataka mashabiki wa Yanga kujitokeza kwa wingi uwanjani kushuhudia timu yao na kuona mpira mzuri wenye ufundi na mbinu.

Naye mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Denis Nkane, alisema wamejiandaa vizuri na wanaenda kuanza ligi kwa kuendeleza walipoishia msimu uliopita kwa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >